
AGOSTI MMXXV - TOLEO LA XLVI

# NGURUMO
*ya Mwandishi*




## PIGA HATUA

**HABARI KUU:**

CHAFAMA chaja na utatuzi wa kero za waandishi?

## YALIYOMO

**TAHARIRI— Uk 02**
'PIGA HAUA'

**MWANDISHI WETU— Uk 03**
ZUBEIR RAZUUR MAVUGO

**NEW IN TOWN: Uk 04** SAN-KARA WA II NA SALAMA BINTI RUBEYA

**PITIO LA VITABU— Uk 05**
KILIO CHETU '45

**SAIKOLOJIA: Uk 06— 07**
UHUSIANO KATI YA UPENDO NA TOFAUTI YA UMRI (2)

**MAKALA: Uk 08 - 09**
MJI MKAVU

**KUTOKA KWA FANANI: Uk 10**
SALUM MAKAMBA ATUFUNZA

**SAKO KWA BAKO – Uk 11**
HANNAN NZAMBA

**RIWAYA: Uk 12—13**
MSALITI '7'

**RIWAYA: Uk 14—15**
Najutia Kuwa Na Wewe '7'

**YA KALE NI DHAHABU: Uk 16**
Alibaba na Wezi 40 '21'

**HABARI MOTO: Uk 17**
CHAFAMA MWAROBAINI WA FASIHI?

**SHUBAKA LA VITABU: Uk 18**
HISTORIA YA VITABU 'BAGHAVAD GITA '

**KITABU NILICHOSOMA: Uk 19**
KOVU LA MOYO

**MATANGAZO: Uk 20**

**MALENGA WA KILEO: Uk 21**
PIGA KURA TANZANIA

**HABARI PICHA: Uk 22**

**KUTOKA MAKTABA: Uk 23**
Maisha ni Mapambano '12'

**ELIMU JAMII: Uk 24 & 25**
SAFARI YA MALEZI— NIDHAMU KATIKA MALEZI

**HADITHI: Uk 26 - 27**
Happy New Year '9'

**HADITHI: Uk 28 - 29**
NGUVU YA KIAPO '04'

## TAHARIRI:
# PIGA HATUA

Ni matumaini yangu kuwa u mzima tena!
Karibu sana katika toleo letu la 46. Mtuwie radhi kwa kuchelewa kutoa jarida hili. Hii imetokana na mwingiliano wa kimajukumu kama ofisi.

Tupo katika mchakato wa marekebisho ya wakati, ili jarida hili liwe likikujia tarehe mosi ya mwezi. Naamini miezi ijayo mbele hilo litawezekana.

Katika toleo hili tumeendelea na mengi ambayo tulikwisha yaanza huko nyuma. Lakini kuendelea huko kunabeba maana nzima ya kupiga hatua. Huwezi kuendelea mbele kama hupigi hatua. Hivyo ujumbe mkuu wa toleo hili ni 'PIGA HATUA'.

Kila mmoja wetu kuna mahali anapotaka kufika kimaisha, na hayo ndiyo maendeleo. Lakini maendeleo hayatakuwa na maana ya maendeleo kama hautapigaa hatua. Ili tuyaite maaendeleo yatupasa tuone umetoka sehemu moja kwenda ya pili na siyo kwenda nyingine. Zingatia 'kwenda ya pili'.

Hivyo basi, katika maisha yako hakikisha unapiga hatua kwenda mbele. Yaani kila mara kuongeza jambo moja zaidi katika yale uliyojipangia kama malengo ya maisha yako.

Asante na nikutakie siku njema!


**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

## MWANDISHI WETU:
## ZUBERY RAZUUR MAVUGO

**Katika toleo hili la 46, tunamleta kwenu Zubery Mavugo. Ingawa kuhusu yeye ilishapwa mwaka 2023, meza ya watozi wa jarida imeona ni vema asomwe tena hasahasa kwa wale wasomaji wapya ambao hawakuwahi kumsoma.**

**Msome umjue...**



Zubery Razuur Mavugo

Jina langu ni Zubery Razuur Mavugo. Nimezaliwa katika kijiji cha Kakola, wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga. Elimu ya msingi nimeipata Kakola na ile ya upili nimeipatia Bulyanhulu Sekondari. Baada ya kumaliza elimu ya upili, mara moja niliingia mtaani na kuanza kujipambania kama wafanyavyo wengi katika vijana wa maisha ya kati.

Historia yangu ya uandishi iko hivi; nikiwa mdogo nilipenda kuandika japo mashairi, sikujua sana kuhusiana na uandishi wa riwaya na kwakuwa sikuwa msomaji wa vitabu, jambo hilo lilikuwa mbali na fikra zangu. Hata nikiwa katika elimu ya upili, bado sikushawishika kuandika vitabu na imani yangu ilikuwa ya kwamba, uandishi wa vitabu vya riwaya ni mahsusi kwa wanazuoni.

Nakumbuka mwaka 2014 nilikuwa Facebook search, niliandika neno, 'Tungo' nikiamini ikisearch nitakutana na washairi ambao ningejenga nao ukaribu. Lakini, isivyo bahati neno 'Tungo' lilinipeleka katika ukurasa mmoja uliyosomeka, 'Tungo za Hussein O. Molito' nikabofya na kuingia kwa kuamini nitakutana na mashairi, isivyobahati nikakutana na hadithi. Nilisoma hadithi kadhaa, kisha palepale nikavutika na kumfuata mwenye kurasa Inbox. Nisifiche, sikuwa nafahamu chochote kuhusu uandishi, huyo bwana ndiye wa kwanza kutumia muda wake kunielekeza misingi muhimu ya sanaa hii na yeye ndiye aliyesema, "Zubery sasa anza kuandika kwa ajili ya jamii" baada ya kuandika nikakutana na Frank Masai mwaka huo, nae akanisaidia sana.

Hawa wawili wakanikosoa bila shufaka, mpaka nikawa mwandishi wa kusomwa.

Nilipita kwa wengi baada yao bila shaka kwako pia nimechukuwa mawaidha na kujifunza, lakini kiufupi safari yangu ya uandishi ilichagizwa sana na mabwana hao. Ingawa Molito ana mambo mengi ya ujana lakini, mie huwa namheshimu sana kwasababu Allah alipenda nipite katika mikono yake.

Nadhani, ni kwasababu napenda kuwa huru katika kujielezea. Sasa, uandishi ni sanaa inayompa fursa mwanadamu kujielezea na kuielezea jamii yake chochote na kwa vyovyote.

Ninawaheshimu waandishi wengi sana, lakini kiukweli mwandishi aliyenivutia zaidi ni Ben. Yeah marehemu, Ben R. Mtobwa nampenda sana. Nivile tu Allah hakuamua niishi wakati wake.

**Mimi nimeandika hadithi kadhaa kama;**


Kisasi Cha Pesa.
Nitakufa Na moyo wangu.
Niende Wapi (Dunia Imenichukia
Nitaanzaje?
Nimekukumbuka.
Nimekuchagua wewe!
Msichana wangu wa kwanza
Kichaa.
Bustani ya Damu.

Licha ya kuugeuza uandishi biashara, pia uandishi umenipa heshIma katika jamii. Kubwa kabisa kuliko vyote ni kwamba, uandishi umenoa kichwa changu kwa kiasi kikubwa sana, nimekuwa mtu wa kujifunza kila siku kisa tu mimi ni mwandishi, Alhamdulillah!

Mwenye uhitaji wa kazi zangu anitafute kwa namba **0759180332** ama anifuate katika Akaunti yangu ya Facebook, InShaAllah nitampa utaratibu wa kuzipata.

Ninachowaambia wapenzi wa kazi zangu ni kwamba, ninawapenda sana na ninawaombea kwa Allah, wanufaike kwa yale ambayo Allah amenijaalia kuwaandalia na kuwafikishia. Isibaki kuwa manufaa kwao pekee bali yalete matokeo katika maisha yao na jamii yao kwa ujumla. Pia, Allah awafungulie milango ya riziki na atie baraka katika upambanaji wao, na muda wote wawe na nyoyo zenye kumkumbuka yeye.


## NEW IN TOWN :
## SANKARA WA II na SALAMA BINTI RUBEYA





**SANKARA WA II**

**kinapatikana TPH BOOKSHOP DAR ES SALAAM kwa Tsh 18,000 tu.**

**Wahi nakala yako usingoje kusimuliwa.**




### Salama binti Rubeya

Simulizi kutoka mwambao wa Bahari ya Hindi

Sasa kipo madukani

**SOMA VITABU KUONDOA UTAPIA MAARIFA**

**Tunaendelea na mapitio ya kitabu cha Kilio Chetu kama kilivyochambuliwa na Mwalimu Makoba.**

**Endelea...**

**MIGOGORO**

**Mgogoro wa nafsi**

Huu ni mgogoro ambao humpata mhusika peke yake kati yake yeye na nafsi yake.

- Suzi anapatwa na mgogoro wa nafsi pale anapopata mimba na kuambukizwa virusi vya UKIMWI. Anabaki akilia, lakini hakujilaumu mwenyewe, bali anamlaumu mama yake kwa kushindwa kumpatia elimu ya jinsia na mahusiano. Katika ukurasa wa 40, anasema,

“Mimi na Joti tungepata bahati ya kuelimishwa tusingetumbu…”

Msimamo

Mwandishi ana msimamo wa kimapinduzi. Katika tatizo la watoto wengi kuangamia kwa ugonjwa wa UKIMWI, anashauri elimu ya jinsia na mahusiano itolewe ili kuleta ukombozi kwa jamii.

**FALSAFA**

Mwandishi anaamini kuwa elimu ya jinsia na mahusiano ikitolewa kwa watoto itawasaidia kupambana na hatari ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI.

**KUFAULU NA KUTOKUFAULU KWA MWANDISHI**

**KUFAULU**

Kufaulu katika fani

- Mwandishi ametumia lugha nyepesi inayoeleweka kwa urahisi.

- Mwandishi ametumia wahusika ambao wameibeba vizuri dhamira kuu

- Mwandishi ametumia muundo rahisi wa moja kwa moja ambao haumchoshi msomaji wala kumchanganya.

**Kufaulu kwa maudhui**

- Mwandishi amefaulu kufikisha dhamira katika jamii juu ya umuhimu wa kuwapatia watoto elimu ya jinsia na mahusiano.

- Pia mwandishi ameifungua jamii na kuionya juu ya hatari ya sayansi na teknolojia endapo itatumiwa vibaya.

**KUTOKUFAULU**

Kutokufaulu katika fani

- Mwandishi ametumia mandhari ya mjini pekee kana kwamba maambukizi ya virusi vya UKIMWI yanawakabili watoto waishio mjini tu.

**Kutokufaulu katika maudhui**

- Ugonjwa wa UKIMWI huwapata watu wote bila kuzingatia umri. Lakini katika tamthiliya hii, wanaougua ugonjwa huu ni watoto pekee. Kwa kiasi fulani mwandishi hajafaulu.

Hata hivyo kazi hii ni bora na inastahili pongezi kwa mafunzo makubwa inayoyatoa katika jamii yetu iliyogubikwa na utandawazi.

***Mwisho***

**PITIO LA VITABU**




www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

SOMA VITABU
- Kwa afya ya ubongo wako
- Kwa kujiongezea maarifa
- Kwa burudani

USISITE
- Kumsimulia mwingine hadithi uliyosoma
- Kumfundisha mwingine yale uliyojifunza
- Kumshauri mwingine kitabu cha kusoma

NI VIZURI
- Kutembelea maktaba
- Maduka ya vitabu
- Kupiga stori na waandishi



Madam Neema mgao

## UHUSIANO ULIOPO KATI YA UPENDO NA TOFAUTI YA UMRI

### FAIDA NA HASARA ZA MAHUSIANO YA WATU WANAOLINGANA UMRI.

### FAIDA.

**Kijamii.**

Zipo faida nyingi kijamii ambapo jamii inazitazama na kuziangazia bila kuziweka kitaalamu, hizi ni faida kikawaida.

**Upendo wa kweli.**

Inaaminika kuwa, mahusiano yanayohusisha kuzidiana umri kwa mmoja wapo huweza kusababishwa na mengi.

**A}. Ugumu wa maisha.**

Ugumu wa maisha umefanya wengi kujiingiza kwenye mahusiano yanayozidiana umri. Jinsia zote yaani *me* na *ke*. Ugumu wa maisha hupelekea mahusiano au ndoa za watu waliozidiana umri. Mwanaume wa miaka 55 akioa binti wa kutoka kwenye familia ya kipato kidogo alie na umri wa miaka 25 hapo hakutokua na mapenzi ya kweli bali hali ya maisha ya binti ndio itakayokua imepelekea ndoa hiyo.

**B}. Tamaa ya vitu vizuri.**

Wakati mwingine, tamaa ya mambo makubwa hupelekea mahusiano ya kuzidiana umri. Kijana wa miaka 25 anaingia kwenye mahusiano na mama mtu mzima wa umri wa miaka 57, mama huyu anampa kijana vitu vile kijana atakavyo, maisha ya anasa, simu ya macho matatu na mengineyo vinaweza kuwa sababu ya kijana kujiingiza kwenye mahusiano hayo. Ni sawa na binti kuanzisha mahusiano na mbaba mtu mzima ili tuu awe akipata pesa ya simu nzuri,maisha mazuri mjini na mambo mengineyo ya anasa.

**C}.Tamaa za kimwili.**

Inaweza kuitwa tamaa ya kimwili au kama kutafsiriwa kuwa kutimiza matakwa ya kihisia aidha potofu au halisi. Ulimwengu wa sasa, vijana wengi wanaamini kuwa na mahusiano na wanawake watu wazima. Sio kwa kutaka mali, hapana. Kijana anaanzisha mahusiano na mama mtu mzima na huduma zote huyo mama mtu mzima anazipata kwa kijana huyo, ni maamuzi ya kijana kuwa amempenda kwa ukweli mwanamama huyo.

Faida kubwa ambayo jamii inapoona watu waliolingana umri wapo kwenye mahusiano au ndoa basi moja kwa moja jamii husema kuwa watu hawa wamependana kweli. Kitu ambacho ni ukweli pia. Hapa pia unaweza kupata wale wapendanao kwa ukweli kabisa *SOUL MATE.*

### WAPENZI HUSIKA WANAKUWA NA AMANI NA HURU

Ukiuondoa utafiti wa kuwa mwanamke ni mkubwa kwa miaka 10 zaidi ya mwanaume, kundi hili linatajwa kuyafurahia mapenzi kwani upo uhalisia wa hisia kati yao bila ulakini wa kitu chochote. Wanakuwa na uhuru kati yao kwani wanalingana umri. Mapenzi ya *age mates* huwa ni matamu na mazuri sana.

### KILA MMOJA ANAUJUA NA KUUTEKELEZA WAJIBU WAKE BILA KUHURUMIWA.

Kundi hili limebeba watu ambao katika umri wao kila mmoja anatekeleza jukumu jake kwa kuwa anautambua vizuri. Katika kundi hili mwanaume anaufanyia kazi uanaume wake ipasavyo na mwanamke anautimi-

za uanaume wake bila kushurutishwa. Kuna ile hali kuwa *"wacha nitekeleze hivi na vile kwani kwanza huyu mwanamke/mwanaume amenizidi umri, lazima niweke heshima ya ukubwa wake lakini pia huyu ni mke/au mume wangu hivyo ni lazima kutekeleza hivi".*

**HASARA.**

Ikiwa kuna faida basi na hasara hazikosekani, tuone kwa uchache.

**A]. HESHIMA HUWA KWA UCHACHE.**

Bahati mbaya watu waliolingana umri kuna wakati kuheshimiana huwa kwa kiwango kidogo, kunakua kama na kadharau kwa mbali kwa kua umri wanalingana. Heshima huwa kwa kiwango kidogo.

**B]. KUTOKUTILIANA MAANANI**

Mazoea huwa kwa kiwango kikubwa sana, kunakua na hali ya kutokutiliana maanani. Kunakua na hali ya kupuuziana, ni kwa kuwa wanalingana.

ASANTE.

The Magic Author,
Queen of psychology.
+255763013206.

**TANGAZO—KWA WAKAZI WA IRINGA**




## UZINDUZI WA KITBU



## 'SALAMA BINTI RUBEYA'

SALMA BINTI RUBEYA ni simulizi kutoka Mwambaao wa Bahari ya Hindi. Kitabu kimengazia historia ambayo kwa kiwango kikubwa haijasimuliwa na mtu wa haiba ya mwandishi huyo Bi. Salha Hamdani.

Pia kinampa sauti mwanamke ambaye anaweza kuonekana hajafanya mambo makubwa kwa viwango vyetu, lakini aliacha alama fulani na kutuachia maisha ambayo yanatupatia funzo.

*(Maneno haya yamechukuliwa kutoka kwenye post ya Ester Karin Mngodo iliyopostiwa tarehe 24/8/2025 Facebbok)*



# SAFARI YA ‘MAJI MANDIGA’ MPAKA ‘MJI MKAVU’

Na Mwandishi wetu

## MJI MKAVU — SIMULIZI YA UKWELI USIOSEMWA | BALAA JIPYA MJINI

**Makala ya leo inakuja tofauti na ulivyozoea. Baada ya taarifa za mshtuko kutufikia katika dawati letu la Ngurumo, kuwa inasemekana kuna Mji Mkavu huko social media, haatukusita kumsaka huyo ‘jambo lake’. Mambo yalikuwa hivi…**

**Huyu si mwingine ni yule yule mwandishi mahiri wa ‘Maji Mandiga’ Mohammed Hammie… hebu tujuze kinagaubaga, kuna lipi katika Mji Mkavu? Na itakuwa vyema tukijua ni vipi ulipataa wazo hili jipya?**

“Mji Mkavu" ni simulizi inayochambua kwa kina changamoto za upatikanaji wa maji katika maeneo ya mijini. Wazo la kuandika kitabu hiki lilinijia baada ya kutambua ukweli mchungu: kwamba si watu wote wanaoishi mijini wanapata huduma ya maji safi na salama kama ambavyo takwimu rasmi zinavyoonesha.

Changamoto hii si ya Tanzania pekee, bali ni taswira halisi katika mataifa mengi ya Afrika. Ingawa taarifa nyingi zinaonesha kuwa hali ya upatikanaji wa maji mijini ni bora ukilinganisha na vijijini, uhalisia unaonesha tofauti kubwa — bado kuna maeneo mengi ya mijini yenye uhaba mkubwa wa maji.
Ukizungumza na wakazi wa maeneo kama Saranga, Goba, Bonyokwa, Mbezi Luis na mengine yaliyo pembezoni mwa jiji la Dar es Salaam, utasikia kilio cha watu wanaoishi na tatizo la maji kila siku, licha ya juhudi kubwa zinazofanywa na serikali na taasisi mbalimbali kuhakikisha huduma hii inawafikia wote.
Katika hali nyingine, uharibifu wa makusudi wa miundombinu ya maji unaofanywa na baadhi ya watu kwa maslahi binafsi, umeendelea kuzorotesha jitihada hizi.

“Mji Mkavu” inakuja kuonesha upande wa pili wa maisha ya mijini — ule upande usiosemwa.

**Asante kwa maelezo haya ya kutosha, lakini kwa faida tu ya wasomaji wetu, hebu tupe walau kifupi kuna nini ndani ya Mji Mkavu?**

### UTANGULIZI | MJI MKAVU

Maisha ya kisasa, hasa katika miji mikubwa, yanaleta faraja nyingi, barabara nzuri za juu na chini, magari yenye viyoyozi, majengo ya kifahari, kumbi za starehe na maduka yaliyojaa kila aina ya mahitaji yetu. Lakini vyote hivi vinaweza kupoteza thamani endapo kitu kimoja kinapokosekana — MAJI.

Tamaa ya pesa ndio mzizi wa maovu yote. Wahujumu wa maji, wale wanaoharibu mabomba makubwa kwa faida zao binafsi, wamekuwa hatari na hakuna anayewapigia kelele. Hivyo maji hupotea tu ardhini pasipo kuwafikia walengwa na kusababisha mahitaji kutotoshelezwa.

Fridah Amani, mwanahabari mwanamke, mwerevu, jasiri na asiyeogopa, anakutana uso kwa uso na ukweli huu katikati ya jiji. Pale anapojikuta akihangaika kutafuta maji, haraka anatambua kwamba hii si shida ya maji kama ile ya maeneo ya vijijini. Hii ni shida bandia, iliyosababishwa na matendo ya kihalifu yanayoathiri maisha ya watu.
Fridah anaamua kuingia vitani, akitumia kalamu yake kama silaha ili kuokoa mji wake usiwe mkavu.

“Mji Mkavu” ni simulizi ya ujasiri na maumivu, nguvu na uvumilivu, inayofichua ukweli mchungu wa changamoto za maji mijini — kwamba hata katika jiji linaloonekana kuwa na raha za kila aina na mafanikio, ukame unaweza kujificha katika kivuli.
*Mwisho*

**Hakika ‘Mji Mkavu’ itasimamisha nchi… hata sasa tayari naona. Enhe *unawapanga* vipi wapenzi wa fasihi?**

Wasomaji wa fasihi ndani na nje ya Tanzania wanapaswa kujiandaa kwa kazi kubwa na ya kipekee itakayobadili namna tunavyoitazama miji mingi barani Afrika. Pia kitapatikana kwa lugha ya Kiingereza chini ya jina *The Dry City*.
Kwa sasa, *The Dry City* iko kwenye hatua ya mwisho ya uhariri, chini ya usimamizi wa

Dylan Groves, Mhadhiri Msaidizi *(Assistant Professor)* kutoka Chuo Kikuu cha Lafayette, Marekani, akishirikiana na Benjamin White kutoka chuo hicho hicho. Ushirikiano huu wa kimataifa ni ishara ya ubora na upeo wa simulizi hii.

Toleo la Kiswahili litakuwa la kwanza kutoka — "Mji Mkavu", ambalo tayari limepata ithibati kutoka Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Hili ni jambo linalotupa matumaini makubwa kwamba kitabu hiki kitafanya vizuri zaidi na kufikia wasomaji wengi baada ya mafanikio ya Maji Mandiga.

Meneja wa kitabu hiki, Mariam Mbano — ambaye pia ni mke wangu — tayari ametambulisha jalada rasmi la kitabu, jambo linaloashiria kuwa muda si mrefu "Mji Mkavu" kitasambazwa rasmi kwa wasomaji.
Kuhusu kama kitabu hiki kitagawiwa bure kama ilivyokuwa kwa Maji Mandiga, hilo ni swali litakalojibiwa rasmi na Meneja siku chache kabla ya kukitoa. Hata hivyo, ni vyema kujua kuwa maandalizi yote muhimu tayari yamekamilika na tumejipanga.

**Mmh! Hongera sana, nasi tunakisubiri kwa hamu. Na haswa tunasubiri neno la Meneja Bi. Mariam Mbano jinsi kitavyopatikana.**
**Lakini vipi mafanikio ya kile Maji Mandiga? Waweza kutueleza au siri ya ofisi?**

Kwa kumbukumbu, nilifanikiwa kupata jumla ya Shilingi milioni 91.3 kupitia Maji Mandiga, ikiwa ni ufadhili kutoka kwa mashirika mbalimbali. Lakini ni imani yangu kuwa "Mji Mkavu" inakuja kuweka historia mpya.

**MAFANIKIO YA KITABU CHA MAJI MANDIGA**

~ Kimepata tuzo ya heshima kutoka mfuko wa Fasihi Tanzania.
~ Kimebadilishwa kutoka simulizi ya maandishi na kuwa KOMIK, kwa maana simulizi kwa mtindo wa michoro. Kwa ufadhili wa shirika la Simavi la nchini Uholanzi.
~ Kimeshinda tuzo nchini Uholanzi kwenye kipengele cha *'creative storytelling for social change'* kupitia shirika la Partos Innovation.
~ Kimeshika nafasi ya pili kwenye tuzo za James Currey Literature nchini Uingereza. Chuo Kikuu cha Oxford.
~ Kimeingia tano bora nchini Nigeria kwenye tuzo za Quramo Writer's Prize.
~ Kimetengenezwa kuwa mchezo wa jukwaani kwa mtindo wa *(Theatre for Development)* Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro (MUM).
~ Kinasomwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kwa wanafunzi wa Bachelor of Art in Literature.
~ Kimesambazwa kwenye maktaba zote nchini Tanzania, kwa maana ya maktaba za mikoa na wilaya. Kwa ufadhili wa shirika la End Water Poverty la nchini Uingereza.
~ Kitabu kipo kwenye hatua za mwisho kwa ajili ya kufanikisha kusomwa shule za sekondari Tanzania chini ya kampuni ya APE.
~ Kitabu kimegawiwa bure kwa wasomaji wote. Hakuna aliyetozwa pesa ya *'delivery',* kuanzia Dar es Salaam na mikoani. Gharama zote zilitolewa na wafadhili.
~ Kitabu kilibailishwa na kuwa mradi: *'Promoting Women's, Girls' and Communities' Spirit to Amplify Their Concerns and Meaningfully Take Action to Improve Water and Sanitation Management through Maji Mandiga boom"* kwa ufadhili wa shirika la Simavi la nchini Uholanzi.
~ Kitabu cha Maji Mandiga kwa lugha ya Kiingereza na KOOMIK kwa lugha ya Kiingereza vimewekwa kwenye tovuti ya shirika la Simavi la nchini Uholanzi kwa mkataba maalum.
~ Kimeshinda tuzo ya Facebook kama kitabu bora cha mwaka 2022-2023.
~ Tumesaini mkataba kwa ajili ya kitabu kuwa filamu. Mpaka sasa *script* ipo tayari, tupo katika hatua ya makubalino ya mgawanyo wa mapato.
~ Kimefanyiwa mjadala kwenye Mkutano wa 10 wa kidunia wa sekta ya maji uliofanyika mjini Bali nchini Indonesia hivi karibuni.

**Aisee! Shukrani sana kwa taarifa hii na hongereni wewe kama mwandishi na Meneja wako uliyemtambulisha kuwa ni 'mkeo'. Basi sisi walaji twaketi mkao wa kula, twasubiri pishi liipuliwe, tule tusaze!**

**Je; unataka kuhaririwa, kuandikiwa (ghost writing), kuhakikiwa au kuchapiwa hadithi au kitabu chako?**

**Wasiliana nasi kwa**
**Whatsapp: 0766974865**
**Call: 0672160016**

SALUM MAKAMBA

## USHAIRI NI BAHARI SI KIJITO - 04-

**USHAIRI NI BAHARI SI KIJITO**

Sehemu ya Nne

Katika sehemu hii ya nne tutatazama namna ilivyo muhimu kuitafuta elimu ya ushairi kwa upana wake ili hata kama kuna misimamo ya utungaji ambayo unaishikilia basi usije ukaona wengine wanakosea. Hata kama misimamo hiyo umeitoa kwa washairi tajika kama Sheikh Msifika Shaaban bin Robert, Sheikh Amri Abeid Karuta, Muyaka bin Haji Al Ghassaniy, Mwalimu Abdilatif Abdallah, Ustadh Amri Sudi Andanenga, Dotto Rangimoto, Prof. Ahmed Sheikh Nabhany au mwingine yeyote yule awaye.

Kwani katika ukurasa wa 55 & 56 wa kitabu cha Kunga za Ushairi na Diwani Yetu (1979) Prof. Mulokozi na Prof. Kahigi wanasema, "Wajibu wetu (sisi tunaotunga sasa) si kukariri kikasuku yale waliyoyasema (hao washairi tajika) na kudai kuwa ndiyo kweli yote kuhusu ushairi wa Kiswahili na anayeipinga "kweli" hiyo ni mjinga, purukushani, mvurugaji n.k."

Na katika kurasa hizohizo wanasisitiza kuwa, uwanja wa ushairi ni mpana sana, hauanzii wala hauishii katika VINA na MIZANI.

Na kama haitoshi wanazuoni hao nguli katika ukurasa wa 56 wanatoa wasia kwa washairi wa Kiswahili kwa kuwaambia, "Wasitosheke na ujuzi walio nao na vilemba vya "ustadh" na "ushaha wa malenga" ambavyo baadhi yao wamevikwa. Vitu hivyo ni ishara kuwa wanatambulikana na kuheshimika katika jamii yetu kuwa ni mabingwa wa ushairi, lakini si uthibitisho kuwa wamefikia upeo wa taaluma ya ushairi na kila walisemalo ni "kweli" na "hekima."

Na ziada ya hilo wanawahimiza pia kusoma na kuendelea kuitafuta elimu ya ushairi kwa kusema, "Wao pia, wanawajibika kujielimisha ama sivyo maendeleo ya fasihi na hasa ushairi yatawaacha nyuma."

Ndiyo maana sisi tuliofunzwa ushairi kwa utulivu na hekima. Tunapoona chochote kinachotutia mashaka basi tunauliza. Hatukurupuki tu na kuanza kuwaita watu wajinga, wasioujua ushairi ama hivi na vile. Kwa sababu tunafahamu kuwa ushairi ni mpana sana. Na tunaruhusu akili zetu zijifunze mapya. Na baada ya kujifunza naweza aidha kukubaliana nayo au kutokubaliana nayo lakini abadani asilani sitampopoa mwenye anayetunga kwani kama ana ushahidi na dalili ya akifanyacho basi hajapotea na yuko katika usahihi wa utunzi wa Kiswahili.

Ni matumaini yangu kuwa wale tulioambatana sote tangu mwanzo hadi mwisho wa mfululizo wa makala hizi kuna jambo kubwa mmejifunza. Nimeandika makala hizi kwa ushahidi wa wanazuoni wawili nguli kabisa wa Kiswahili nchini akiwemo Prof. M.M Mulokozi. Ambaye nimemtumia kwa kusudi maalum kabisa.

Nihitimishe kwa kusisitiza kuwa, ushairi wa Kiswahili si vina na mizani, idadi ya beti au aina fulani ya bahari. Bali uwiano baina ya fani na maudhui. Na muunganiko wa fani na maudhui ndiyo SHAIRI. Asiyetaka kuamini katika haya sina shida naye. Aamini hivyo anavyoamini ila katu asije kuwanyooshea vidole wasioamini kama yeye kwa kuwaambia kuwa hawajui kutunga au wameshindwa kutunga ndiyo maana wanasema wanayoyasema. Kwani hata sisi si yetu bali ni mafuhumu ya wanazuoni kama nilivyofafanua tangu mwanzo hadi mwisho wa makala haya.

Chambilecho Joram Nkumbi, wabaadu wakatabahu fakiri, nayayuka huku nikiweweseka kiwendawazimu.

MWISHO

Muhimu:

**Endelea kujipatia Diwani iliyoshinda Tuzo ya Afrika mwaka 2022/23, Mamangu Nipe Wosia pale TPH Bookshop Posta jijini Dar es salaam.**

## SAKO KWA BAKO:

## HANNAN NZAMBA: MUASISI WA KONA YA RIWAYA BOOK CLUB

**Leo katika safu yetu ya Ana kwa Ana tumemrejelea mwanadada mrembo, mcheshi na mwenye maneno mengi sana. Kwa kuwa nitakuwa na mazungumzo mengine marefu na yeye, na yatakujia hapa, nikaona nikurudishe kwanza kwenye toleo la nyuma ambapo yeye mwenyewe alitueleza machache tu.**

**Ilikuwa mwaka 2023 mwezi Machi… nilianza hivi;**

Mwanadada huyu ilinibidi kumtafuta baada ya kusikia habari zake kuwa ni muasisi wa Kilabu cha wasoma vitabu 'Book Club' cha Kona ya Riwaya. Nikaona isiwe tabu hebu atuambie mawili matatu kujihusu na kuhusu hilo afanyalo. Karibu!

**Tuanze kukufahamu kwanza...**

Naitwa Hannan NZAMBA. Ni mtoto wa nne kwenye familia yetu yenye watoto 6. Mimi ni mama wa watoto watatu. Mi nimezaliwa hapahapa Dar es salaam huko Ada Estate.

Shule ya msingi nimesoma Mbuyuni na sekondari nimesoma Loleza Mbeya. Mimi ni mjasiliamali ninayefanya shughuli zangu ndogo ndogo za kuniingizia kipato

Mimi katika maisha yangu nilipenda sana kuwa *Pilot*. Wala sikutaka kuwa mwandishi ila ni mapenzi yangu tu kwa vitabu ndiyo yaliyoleta wazo la kuanzisha hii Book Club.

**Sasa nini kilikusukuma kuanzisha kilabu hiki?**

Kilichonisukuma ni mapenzi kwa vitabu.

Chimbuko la kila kitu ni Loleza Secondary, pale alikuwapo mwalimu anaitwa Mwl. Mwakasege alikuwa ni mwalimu mzuri sana wa Kiswahili (*Sijui kama yupo hai au la…)*. Yeye ndiye aliyenifundisha haya mambo ya uchambuzi wa vitabu. Kila nikifunga shule ananipa kitabu niende nacho nyumbani na shule ikifunguliwa nije nimwelezee kuhusu kitabu hicho.

***Mpaka sasa kuna matokeo gani uliyoyaona kupitia kilabu hiki?*** Bado sijaona matokeo kwa sababu ndio kwanza tunaanza. Ila malengo yangu ni watu wapende kusoma vitabu. Mi naamini kuna mambo mengi sana ya kujifunza kwenye vitabu. Hata mwanao utamfundisha kusoma na akipenda kusoma, thamani ya vitabu itaonekana.

***Mpaka sasa mmekwishachambua vitabu vipi?*** Mpaka sasa tumeshafanya uchambuzi wa vitabu kama cha;

Adam Shaffi - mtoto wa mama
Laura Pettie- kiroba cheusi
Fadhil Mtanga - Fungate
Mfadhili - Hussein Tuwa
Ibrahim Gama- barua kutoka jela
Hussein Molito - Chawa
Maundu Mwingizi - Kitanda cha kuwadi
Frank Masai - Mwimbula

**Na, bado mnaendelea au?**
Bado tunaendelea na mikutano yetu ya uchambuzi hivyo tunapenda kuwaalika watu wafike kwa wingi tujifunze kupitia chambuzi hizi.

**Asante sana kwa haya machache, natumai wakati mwingine tutapata muda wa kuzungumza mengi zaidi.**

Asante sana ndugu mwandishi



# MSALITI - 07

Na. Richard Mwambe

**Ilipoishia ...**

**Inawezekana kwenye hayo makontena kuna mizigo isiyo halali kwani hawakukuambini kuna nini?" akahoji."Ile mizigo ni vyombo vya nyumbani tu…" Gina akadakiza.**

**"Heh! Vyombo tu aaaaa au na nyie mna mkono mfupi?" yule mkurugenzi akauliza baada ya kushangaa.**

---

"Ninyi mnajua wazi kuwa kama ni vitengo vyenye rushwa bandari inaongoza hata huyu Besta alishawahi kuandika madudu ya pale…"

"Enheeeee… na ndiyo maana tumekuja!" Gina akamkatisha kabla hajamaliza.

"Ok! Aaa sasa shida ni moja huyu jamaa siyo Mtanzania, na watu wengi hawajui hilo," yule mkurugenzi akawaambia kwa sauti ya chini.

"Siyo Mtanzania?" Amata akauliza.

"Yaani amechangia, baba ni wa Burundi na mama ni wa Kagera huko," akawaeleza. Gina akatikisa kichwa juu chini. Yeye aliwahi kufika hapa ofisini mara mbili tu, nina karibu mwaka na kitu tunawasiliana kwa simu tu. Habari zote hizi huwa anatuma kwa barua pepe…" akaeleza.

"Mara ya mwisho umempigia lini?" Amata akauliza.

"Ni kama juma moja limepita, jana nimemtafuta sana lakini sijampata kabisa," akajibu huku akichukua simu yake na kuanza kubofya namba kadhaa ili kumtafuta. *'Namba unayopiga haipatikani kwa sasa'* ndivyo simu ile ilivyojibu. "Hapatikani huyu sijui ana shida gani!" yule mkurugenzi akasema huku akijiweka vizuri kitini.

"Na haishi Dar'?" Amata akauliza.

"Hapana, haishi Dar' na kwa sababu ya kazi yake basi huwa anazunguka zunguka sana," yule mkurugenzi akajibu kwa ufasaha kabisa asijue ni nani walio mbele yake. "Nyie pale wekeni pesa tu mambo yataenda… wahenga walisema penye uzia penyeza rupia…"akawaambia na kufuatia na kicheko kizito.

"Tunaweza kupata namba yake?" Gina akauliza.

"Ooh bila shaka, bila shaka…" akajibu na kuvuta mtoto wa meza, kisha akatoa kadi kazi na kuwapatia. Gina aliipokea na kuisoma, kisha akampatia Amata. *Besta Ekolaneza!* Akasoma kwa sauti ya moyoni asiyoisikia mtu isipokuwa yeye na malaika wake. Baada ya mazungumzo hayo mafupi waliagana. Gina na Amata wakarudi ofisini kwao, AGI Investment katika jengo la JM Mall.

"Atakuwa ni huyu kweli?" Amata akauliza.

"Inabidi tu kupiga ngumi kichakani…" Gina akajibu.

"Sasa kama ni hivo inabidi tuanze kuchora ramani ya vita… jambo kubwa ambalo nataka nijue, ni kwamba alitaka kunipa habari gani?"Amata akasema huku akivuta kitabu chake cha kumbukumbu na kuandika mambo fulani.

"Kwahiyo tunaanzia wapi?" Gina akauliza. "Na safari hii huendi peke yako mana kama ni kazi basi hii ni ya kujitakia, bibi yako hayupo…" akaongea kwa kumaanisha. Toni ya kauli yake ilibeba kila chembe ya wivu.

"Tunaenda wote, sasa andaa safari ya Mwanza. Tutatua Mwanza halafu tutaanza safari ya kwenda Ngara," Amata akamwambia. "Angalia ndege ya kesho, leo kuna watu nataka nikabiliane nao kuna jambo nahitaji ufafanuzi kidogo," akaongeza kusema.

"Jambo gani tena?"

"Kuna hii ishu ya JW, hawa jamaa waliouawa huko Beni… kuna maswali kadhaa ambayo yananinyima raha, nahitaji kuyajua majibu yake," Amata akaeleza.

"Unaende kwa nani?" Gina akataka kujua.

"Naenda kwa CDF mwenyewe," Amata akajibu wakati tayari uko wima kwa safari.

❦

Siku hii mkuu wa majeshi au CDF alikuwa ofisini kwake kimya kabisa. Kiujumla hakuwa tayari kupokea ugeni wowote ule. Kichwa chake kilisawajika kwa mawazo. Kuondokewa na vijana wake kumi na nne halikuwa jambo dogo hata kidogo. Kamanda Amata aliwasili makao makuu ya jeshi hilo na kuegesha gari panapotakiwa. Akateremka na kuiweka tai yake vizuri, kisha akavuta hatua kuelekea jengo la utawala lililokuwa mita chache tu kutoka pale alipoegesha gari lake. Akavikwea vidato vichache vya ngazi kuuelekea mlango. Alipokuwa akipandisha mguu wake wa kulia kumalizia kidato cha mwisho cha ile ngazi akajikwaa ncha ya kiatu chake na kutaka kuanguka. Lakini utimamu wa mwili wake haukuruhusu hilo kutokea.

"Pole kaka!" kauli hii ilisikika kutoka nyuma yake. Alipogeuka alikutana macho na mwanadada aliyevalia suti ya gharama. Suti ile ilionesha wazi uwezo wa kipesa

alionao na ilimtambulisha moja kwa moja kuwa ni katibu muhtasi katika ofisi ile anayoiendea Amata.

"Asante sana mrembo! Natumai niliyemfuata nimemkuta…" akasema.

"Una shida na nani?" yule mwanadada akahoji.

"Nina shida na Jenerali…" akasema pasi na kumtaja jina lake.

"Nikikwambia hayupo… je?"

"Utakuwa umenidanganya…" Amata akamjibu yule mwanadada.

"A hahahahaaaa… kwa nini?"

"Si unaona nimejikwaa mguu wa kulia! Maana yake ninayemfuata yupo au ninachokifuata kipo…." Amata akajibu huku akimfuata kuingia katika ofisi ile nadhifu ambayo yule mwanadada aliingia.

"Ahahahahaaa… ah! Usinichekeshe mie! Imani za wapi hizo? Jenerali wala hayupo leo, si unajua ana msiba," yule mwanadada akamwambia Amata huku akiwa ametingwa na kutafuta kitu fulani kwenye droo ya meza yake.

"Hujanidanganya bado, mi nikijikwaa mguu wa kulia basi kile kitu ni sawa ila wa kushoto ndiyo huwa kinyume!" akafafanua.

"*Anyway*… wote nimewaambia hayupo na ndiyo maagizo niliyopewa, ila kwa imani yako unanifanya nikuogope. Jenerali yupo ila hutoweza kumwona kwa sasa au niseme kwa juma hili lote!" yule mwanadada akamwambia Amata wakati akiiweka sawa kompyuta yake na kusogeza moja ya nyaraka muhimu sana iliyokuwa juu ya meza yake. Mwanzo Amata hakuitilia maanani lakini kitu kimoja alichokiona kwenye ile karatasi kilimfanya amakinike nayo. Karatasi ile ilikuwa na orodha ya majina. Pasi na shaka, yalikuwa majina ya wale marehemu, vijana wa jeshi. Majina yale yalikuwa kumi na nne. Chini ya hayo kumi na nne palipigwa mstari mwekundu, halafu yakafuata mengine mawili. Chini ya hayo mawili tena pakapigwa mstari mwekundu, halafu yakafuata mengine kama ishirini hivi. Katika taarifa iliyoandikwa juu ya vifo vile, iliesema, wanajeshi waliokufa na kutambulika ni kumi na nne; wawili hawakutambulika kutokana na miili yao kuungua vibaya na waliojeruhiwa ni ishirini na moja. Na kweli, kulikuwa na masanduku kumi na sita. Ilimaanisha kuwa wanajeshi theluthi moja ya Watanzania walikufa, waliobaki walikuwa hoi bin taabani hospitalini.

"Nina shida nyeti sana kwake, najua ukimwambia Kamanda Amata ana shida naye, bila shaka atakuelewa," Amata akasema. Yule mwanadada akainua sura yake na kumtazama kwa jozi la sekunde. Kisha akatikisa kichwa na kurudisha macho yake kwenye ile kompyuta pale mezani.

"Siyo rahisi kama unavyofikiria…" akaendelea kucheza na baobonye la ile kompyuta pasi na kumwangalia huyo aliyesimama mbele yake. "Jaribu!"

"Siwezi, atanikaripia na mimi sipo tayari kuharibu siku yangu," yule katibu muhtasi akamjibu Amata. Kisha akaichukua ile karatasi na kuitia ndani ya kabrasha jingine.

"*Anyway,* ngoja nimpigie!" Amata akasema na kuchukua simu yake tayari kufanya kazi hiyo. Yule mwanadada akabaki anamtumbulia jicho kijana huyo hasijue nini cha kufanya.

"Hello!" akaita.

*"Hello… naongea na nani?"* sauti nzito ikapenya katika masikio ya Amata.

"Spark…" akajibu.


*"Unaasemaje?"*

"Ninahitaji kukuona nina ujumbe wako kutoka Namba Moja!" Amata akasema.

*"Pita ndani!"* ile sauti ikamjibu. Amata akakata simu na kumtazama yule mwanadada.

"Nipeleke!" akamwambia.

***Itaendelea...***




Kitabu MSALITI kipo madukani, jikamatie nakala yako kwa Tsh 15,000 tu.

Tembelea duka la Kona ya Riwaya Kinondoni au piga

**simu namba 0655428085**
**Whatsapp 0766974865**

Jikamatie nakala yako sasa

# HADITHI: Najutia Kuwa na Wewe—06

MTUNZI: ASHA SIRAJ
Whatsapp 0789044345



**UTANGULIZI**

**Mapenzi sio kitu cha kuwekea maanani sana kwasababu ipo siku yanaweza kukuletea shida huko mbeleni, kuna baadhi ya changamoto nyingi hutokea. Hivyo ukisema kila jambo uliwekee maanani basi mapenzi yako yatabaki kuwa na majuto siku zote. Kutana na binti SHAZMA aliyepitia mateso mengi kwenye mapenzi yake na kujikuta akijutia kwanini amkabizi moyo wake mwanaume asiye na fadhila**

***Ilipoishia…***

**Nilisogea hadi sehemu nilipokuwa nalala nilipanda ngazi kuelekea kitanda cha juu kabisa maana yeye alikuwa analala mwanzo kabisa huku katikati alikuwa analala Judithi mwisho nilimalizia mimi.**

***Endelea...***

Nilivuta shuka langu nakujufunika huku nikajirabu kuutafuta usingi mnono, ila chakushangaza siku hiyo ilikuwa siku nzito mimi kupata usingizi. Nilihisi huenda wanga wananiwangia. Si unajua sehemu zenye watu wengi hazikosagi mambo hayo, au huenda akawa huyo Catherine nini? Nilijiuliza ila sikuwa na majibu ya maswali yangu.

Niliamua kusoma kisomo pale ili niweze kupata usingizi na ukiangalia muda ulikuwa umeenda sana.

Baada ya kufanya kisomo pale nilijifunika shuka hadi kichwani, ila moyo wangu ulijawa na wasiwasi na sikujua nini tatizo.

Kama ni kisomo, tayari nilifanya, lakini nini shida hadi mimi kuwa hivi. Sikupata jibu, nilihisi kama kulia hivi; yaani nilitamani nilie ila sikutaka kuwapigia kelele waliokuwa wamelala.

Mpaka kuna kucha nilipitia wakati mgumu sana, macho yangu yalikuwa mekundu kwa ajili ya kukosa usingizi

Asubuhi kulipokucha kila mmoja alikuwa ananiuliza macho yangu yana shida gani? Mbona yamekuwa mekundu gafla.

Judithi alijibu kabla hata mimi sijaongea, "mnauliza jibu kwanini yamekuwa mekundu kwani jana hamjamuona kama alikuwa *busy* na kujisomea! Mwenzetu anataka kuwa rais".

Hivi huyo judithi nimfanye nini mimi, natamani angejua nini kilitokea jana usiku basi asingeweza kuongea maneno hayo.

Niliondoka zangu pale bila kuwajibu nikaelekea darasani. Siku hiyo ilitakiwa tuingie darasani mapema kwa ajili ya kipindi cha asubuhi

Judithi alinifuata kwa nyuma akiwa ananihoji? "Shazma ni kwamba umenuna kwasababu ya maneno yangu? Nilikuwa natania rafiki yangu hivyo naomba usiniwazie vibaya tafadhali".

"Judithi kuna wakati unatakiwa upunguze matani yako ila siwezi kukulaumu ndivyo umejizoesha mwenyewe

Ila usijali kununa kwenyewe sijui, ila leo siko sawa toka jana usiku sijielewi kabisa sijui kuna tatizo gani. Jamani" nikamweleza.

Haya tukiwa darasani tunapiga stori mbili tatu mimi pamoja na Judithi huku wanafunzi wengine wakiwa *busy* na kujisomea

Mara mwalimu aliingia darasani tukawa tumeacha kupiga stori maana nilitaka kumwambia Judithi kile ambacho kimetokea usiku

Tulianza kipindi cha asubuhi huku moyo wangu ukiwa bado umejawa na wasi wasi mkubwa hata kile alichokielezea mwalimu mbele sikuwa naelewa kabisa.

Niliona kama ananipigia kelele kwenye masikio yangu tu, nilitamani aondoke walau niweze kupumzika kidogo kwasababu macho yangu yalijawa na usingizi.

Tukiwa darasa ghafla hodi ilisikika mlangoni, hakuwa mwingine bali alikuwa mwanafunzi mwenzetu ila yeye alikuwa anasoma kidato cha tatu, mimi kipindi hicho nilikuwa kidato cha nne tulikuwa na miezi michache kuhitimu pale.

Basi mwanafunzi yule aliingia darasani, sikujua nini amemwambia mwalimu ila nilisikia jina langu likiitwa na pale "shazma".

"Abee teacher!" niliitika huku nikinyanyuka na kutaka kumsikiliza nini anataka kuongea, "unaitwa na

mkuu ofisini kwake”. *Mungu wangu nini kimetokea tena huko, nimefanya kosa au?* Nilijiuliza mimi kama mimi.

Nilinyanyuka kuelekea ofisi kwa mkuu, nilipofika nilimsalimia na kutaka kujua nini kinaendelea.
“Shazma!” aliinita kwa sauti ya huzuni sana. “Sikuta kuliongelea jambo hili ila sina namna inanipasa nikupe taarifa hizo japo ni za kusikitisha ila sina namna yakuendelea kukuficha ikiwa wewe ni mwana familia”.
Nilipokuwa nimesimama nilianza kutetemeka ghafla, “pole sana Shazma ila ukweli ni kwamba hatunaye tena anko wako Jamary... amepata ajali leo asubuhi wakati anaenda kazini”. Yani kabla mkuu hajamaliza kuongea mimi pale pale nilidondoka chini na kupoteza fahamu.

Nilikuja kuzinduka nipo hospitali sikujua nini kilijiri pale ila wakati nafungua macho yangu, nilishangaa kuiona sura ya Shahdu mbele yangu akiwa amevalia sare za kidaktari.
*Ina maana shahdu ni daktari, kwanza ilikuwajekuwaje hadi nikawa hapa?* Nilianza kukumbuka, mara ya mwisho nilipoitwa na mkuu ofisini na kupewa habari za msiba.
Nilianza kulia upya pale nilipokumbuka siko na *anko* wangu tena. Machozi yalianza upya nilipiga kelele nakumuita mjomba Jamary.

“Shazma nini shida?” aliongea Shahdu huku akiwa ananikaribia, nililia sana nikashindwa cha kumjibu. Alibaki kufuta machozi yangu kwa huruma
“Huu ni kama mkosi Shahdu, hata yule niliyekuwa karibu naye amechukuliwa, maisha yangu yamekuwa maisha ya manyanyasiko siku zote wapi nitampata mtu kama mjomba jamary.”

Nililia sana na ukiangalia bado nilikuwa nimetundikiwa dripu ila mimi sikujali kabisa nilitamani hata mimi nimfuate huko huko alikoelekea mjomba Jamary.

Nililia sana na ukingalia usiku wa jana sikuweza kulala vizuri hivyo macho yangu yalidhidi kuwa mekundu nikimuomba dokta Shahdu walau aniruhusu nikashiliki kwenye maziko ya mjomba Jamary.
Ila hakutaka kunisikiliza nilisubiri alipoweza kutoka nilianza kuchomoa dripu huku nikitafuta mbinu ya kutoroka pale ili niweze kuwahi mazishi ya Anko Jamari
Wakati bado sijamaliza, ghafla mlango wa wodi ulifunguliwa, hakuwa mwingine bali alikuwa Shahdu.
“Nilijua, Shazma ubishi wako unaweza kufanya kitu kama hiki,” aliniambia.

Niliogopa sana na kuanza kutetemeka. Nikabaki kuomba samahani tu pale, “naomba unisamehe sana dokta ila sikuwa na nia ya kufanya hivi, nampenda sana mjomba wangu hivyo natamani nimuone kwa mara ya mwisho”.

“Ila kwa sasa bado mwili wako haujatengamaa vizuri hivyo unatakiwa kukaa hapa mpaka pale hali yako itakapokaa sawa”.

“Dokta unaongea tu. ni kwa sababu hujui maisha yangu ila jua kabisa yule ndio alikuwa kila kitu kwenye maisha yangu.
Kwa sasa ni kama nimepoteza ndoto zangu za maisha sijui niwapi nitaelekea mimi,” nikaanza kulia upya.


“Shazma acha kusema hivyo Mungu ndo anayejua nini anapanga kuhusu maisha yako. Wewe kwa sasa ni kama rafiki yangu unaweza kunielezea nini kinakusumbua mpaka kusema hivyo”.

Nilitamani nimueleze Shahdu maisha yangu ila hata nimueleze kitu gani hatonisaidia zaidi ya kuuchosha mdomo wangu kuelezea maisha yangu.

“Please Shazma naweza kusema niko hapa kwa ajili ya kusikiliza naweza nikakusaidia chochote kile ambacho ninawezana nacho” akanibembeleza.
Niliwaza sana, ndo kusema naenda tena kupitia maisha yale yale kwa shangazi. Wewe! Niliamua kuufumbua mdomo wangu na kuanza kumuelezea jambo moja baada ya jingine kuhusu maisha yangu.

Japo sikuwa namjua kiundani zaidi ila yeye niliona anaweza kuwa msaada kwenye maisha yangu. Nilimuelezea huku nikiwa nalia sana, kwasababu nilishindwa kuyazuia machozi yangu kwa kile ambacho nilikipitia hapo mwanzo.

*Itaendelea...*



# Ya Kale Ni Dhahabu– Alibaba na Wezi 40 (20)

***Ilipoishia…***

**Marjane akaanza kupiga dufu taratibu na kuanza kucheza akizunguka chumba kile huku akitabasamu.**

**Alibaba na mgeni wake wakaanza kupiga makofi na mke wa Alibaba na mke wa Kassim wakaanza kuimba. Khalid alisimama dirishani akitabasamu tu.**

*Endelea…*

Kisha Marjane akaanza kucheza haraka haraka. Alionekana kama anataka kupaa. Gauni lake lilikuwa likizunguka kama mwamvuli. Alishikilia dufu juu kupita usawa wa kichwa chake na kulitikisa ili vikengele vidogo vya kwenye dufu lile vitoe sauti. Kisha, kwa mkono wa pili, akatoa kisu kilichopo kwenye ile ala aliyoifunga kiunoni kwenye mkanda. Akaonesha kama ishara ya kukatakata vitu hewani, zote hizo ni mbwembwe mbalimbali za uchezaji.

Akaendelea kucheza mpaka akaenda kwa Alibaba na kujinyooshea kile kisu kifuani kwake mwenyewe na kisha kumnyooshea bosi wake. Akaendelea hivyohivyo kucheza mpaka kwa mke wa Alibaba na kwa mke wa Kassim, na kisha kwa Khalid.

Akazunguka na kunyoosha kisu kile hewani juu na kuendelea kucheza.

Kisha akacheza mpaka kwa Khoja Hussein na kumyooshea kisu kama alivyofanya kwa wengine huku akishusha dufu lile chini na kulishikilia kama sahani.

Alibaba alicheka na kutumbukiza baadhi ya sarafu za dhahabu kwenye lile dufu aliloshikilia Marjane.

"Unastahili kabisa kupata dhahabu hizi! Marjane" Alisema Alibaba. "Umetuburudisha vizuri sana jioni hii."

Marjane huku ameshikilia dufu lile kama sahani ya chakula, akaendelea kucheza tena mpaka kwa wake wawili, nao wakatumbukiza sarafu za dhahabu katika dufu lile. Kisha ikawa ni zamu ya Khalid. Khalid alitabasamu wakati Marjane akimtazama na Khalid akatumbukiza sarafu za dhahabu kwenye dufu lile.

Mwishowe akafika kwa Khoja Hussein, Marjane akamuelekezea lile dufu.

Kiongozi wa wezi alitabasamu na kuingiza mkono wake mfukoni ili naye atoa japo sarafu kidogo kama wenzake walivyofanya. Muda uleule, Marjane akanyanyua kisu chake juu hewani na, kwa nguvu zake zote alikisukuma kisu kile mpaka kifuani mwa Khoja Hussein.

Khoja Hussein akaanguka nyumba ya sofa. Alibaba na Khalid wakakimbia haraka kwenda kumsaidia.

Alibaba akaweka mkono wake mdomoni kwa Khoja Hussein kuona kama anapumua, na kisha akashika kiganja chake ili kuona kama mapigo ya moyo yanaendelea.

"Hapumui tena!" Alifoka Alibaba. "Na moyo wake umesimama! Amekufa!! Wewe muovu, msichana muovu kabisa!! Kwanini umemwua??"

Kisha Marjane akausogelea mwili wa Khoja Hussein na kuchomoa ule upanga uliokuwa umejificha kwenye koti. Akamuoneshea Alibaba.

"Hakuja kukutembelea." Marjane alimwambia Alibaba. "Alikuja kukuua. Nimeokoa maisha yako tena bosi."

"Alikuja kuniua?" Alibaba aliuliza kwa mshangao mkubwa sana. "Kwanini rafiki wa mwanangu Khoja Hussein aje kuniua?"

"Huyu sio Khoja Hussein." Marjane alielezea. "Huyu ni yule kiongozi wa wale wezi thelathini na tisa. Ametaka kukuua muda mrefu sana. Huyu ni yule muuza mafuta ambaye alikuja hapa kabla – na ni muuaji huyu!"

"Kiongozi wa wezi? Wezi waliomuua kaka yangu? Lakini umejuaje Marjane?" Alibaba aliuliza. "umemtambuaje?"

"Uliponiambia kwamba hali chumvi, nikaanza kumtilia mashaka," Marjane alieleza.

"Nikakumbuka usemi wa zamani wa wazee wetu ukisema: ukitaka kumwua mtu, usile chumvi nyumbani kwake. Hivyo nilipoenda mezani kutenga chakula nikamuangalia usoni kwa umakini kabisa, nikamtambua kuwa ni yule yule muuza mafuta ila amebadilika kwasababu amenyoa upara na ameweka ndevu za bandia, pia nikaona upanga ameuficha katika koti lake. Unaona sasa! Nilikuwa na uhakika kabisa kuwa ndiye mwenyewe"

Alibaba alifurahi sana kusikia hivyo.

"Marjane, umeokoa maisha yangu tena," alisema. ***Itaendelea...***



# CHAFAMA: Chama cha Fasihi na Maendeleo
# Je; Kitakuwa Mwarobaini wa Kero za Waandishi Bunifu Tanzania?

Na Mwandishi wetu

Kuanzishwa kwa CHAFAMA yaweza kuwa ni faraja kwa waandishi bunifu hapa nchini. Akizungumza na mwandishi wa Jarida hili, muasisi na Mwenyekiti wa CHAFAMA Bi. Eva Mrema alieleza kuwa chama hicho kimeanzishwa kwa lengo la kutambua, kuthamini, na kuwawezesha waandishi wa vitabu nchini Tanzania, hasa wale wanaotegemea uandishi kama chanzo pekee ama kikuu cha mapato ya kuendeshea maisha yao, pia waweze kufanikisha maendeleo yao binafsi na kuchangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya taifa letu la Tanzania.

Alipokuwa akijibu swali kutoka kwa mwandishi wa Ngurumo, Bi. Eva Mrema alieleza kwamba CHAFAMA ni mayokeo ya nutafiti mdogo alioufanya kwa kushirikiana na waandishi waliobobea katika tasnia hii kwa muda mrefu. Kupitia mawazo yao na uzoefu wao wa kiutendaji, amefanikiwa kuanzisha chama hiki ambacho annaamini kitakuwa chombo madhubuti cha ukombozi na maendeleo kwa wanafasihi wote.

Kauli mbiu ya CHAFAMA ni Fasihi kwa Maendeleo ya Mwandishi na Taifa ambayo inaakisi imani yetu kuwa mafanikio ya mwandishi mmoja mmoja ni sehemu ya mafanikio ya taifa kwa ujumla. Aliongeza kwamba kwa msingi huo, CHAFAMA kinalenga kuimarisha uwezo wa waandishi na kuwajengea mazingira rafiki ya kazi na masoko ya kazi zao.

Chama hicho tayari kimejitambulisha rasmi kwa taasisi muhimu za serikali na wadau wakuu wa lugha na fasihi, zikiwemo: BAKITA – Kwa ushirikiano katika kukuza na kulinda lugha ya Kiswahili. Lakini kama mlezi wa wanafasihi, COSOTA – Kwa masuala ya haki miliki za waandishi, MAKTABA KUU YA TAIFA – Kwa utunzaji wa kazi za fasihi. Pamoja na wadau wengine wa kitaifa na kimataifa.

Aidha Bi. Eva alieleza kuwa kwa sasa, CHAFAMA kina wanachama wachache waliotambuliwa kama wanachama waanzilishi kulingana na katiba yake.

Katika kujibu swali jingine kuhusiana na hiarakia ya uongozi wa chama hicho, alieleza kuwa uongozi wa chama unaundwa na waandishi wenye kiu ya kukua na kubobea katika fasihi. Ni waandishi wenye dira ya kuendeleza tasnia ya uandishi kwa weledi na maadili.

Imani ya CHAFAMA ni kuwa mafanikio ya mwandishi yanapatikana kwa njia ya mshikamano na ushirikiano wa kweli. Muasisi huyo ametoa wito kwa vyama vingine vya kifasihi na taasisi kama UWARIDI, UWAVITA, CHAKITA, TATAKI, UKUTA na BAKIZA, kushirikiana nacho katika kuimarisha tasnia ya uandishi wa vitabu nchini.

Misingi ya CHAFAMA imejengwa katika maadili ya Umoja, Uwazi, Ushirikiano, Uadilifu, Uwajibikaji, Uhuru, Heshima na Usawa ikijikita kwenye kuwawezesha waandishi ndani na nje ya nchi ili kutoa kazi bora, zenye mchango mkubwa kwa maendeleo yao binafsi na ya taifa kwa ujumla.




Pichani: Bi. Eva Mrema (kulia) akiwasilisha barua ya utambulisho wa CHAFAMA kwa ..... Wa COSOTA

# HISTORIA YA VITABU ULIMWENGUNI—6

Katika toleo hili la 46 tunaendelea kucjambua historia ya vitabu ulimwenguni. Hapa tulipo ni sehemu ya 6 na baada ya kumalizana na kitabu cha Egyptian Book of the Dead, sasa tutakiangazia Kitabu cha Bhagavad Gita.

## BAGHAVAD GITA

### Historia: Asili yake katika Mahabharata

Baghavad Gita ni sehemu ya epic kubwa ya Mahabharata, mojawapo ya hadithi ndefu zaidi duniani. Mahabharata iliandikwa na Vyasa (Vedavyasa), mwandishi na mwanafalsafa mkuu wa India ya kale.

Gita ipo katika kitabu cha sita cha Mahabharata (Brisma Parva), sura ya 23 - 40.

### Muktadha wa Hali

Hadithi hii inatokaea katika vita vya Kurukshetra, vita vya ndugu wa kifalme kutoka koo mbili: Pandava na Kaurava. Kabla ya vita kuanza, shujaa Arjuna anapata mashaka ya kimaadili: "Je ni sawa kupigana vita na kuua ndugu zangu, walimu wangu na marafiki zangu kwa ajili ya ufalme?"

Hapo ndipo Krishna, rafiki yake na dereva wa gari lake la vita, anamfundisha falsafa ya kiroho - ndiyo maandishi tunayoyaita Bhagavad Gita.

### Iliandikwa Wakati Gani?

Wanahistoria wa maandiko ya Kihindu wanakadiria kuwa Gita iliandikwa katika karne ya 5 KK hadi karne ya 6 KK. Ingawa Mahabharata yote ilikusanywa kwa karne nyingi, Gita yenyewe inaonekana kuwa sehemu ya mapema zaidi, iliyoingizwa ili kutoa mwongozo wa kiroho katikati ya simulizi ya vita.

### Mafundisho Yake Kihistoria

Gita ilionekana kama jaribio la kupatanisha njia taatu kuu za Kihindu.

1. **Njia ya Maarifa (Jnana Yoga)** - kutoka falsafaa ya Vendata.
2. **Njia ya Matendo (Karma Yoga)** - kufuata wajibu na sheria za kijamii.
3. **Njia ya Ibada (Bhakti Yoga)** - kumuelekea Mungu kwa imani na upendo.

### Mafundisho mengine

- **Mungu na nafsi (Atman na Brahman)**
  Nafsi ya mwanadamu (atman) ni ya milele na hufaulu kuungana na ile roho kuu ya ulimwengu (Brahman au Paramatma)

- **Kutokufungamana (Detachment)**
  Mwanadamu anatakiwa kutenda wajibu wake bila tamaa ya matokeo, akimuachia Mungu matunda ya kazi yake.

Hivyo Gita imekuwa kama daraja kati ya falsafa za kale na harakati mpya za kiroho.

**Umuhimu Katika Historia**

Katika nyakati za kisiasa, Gita iliwahi kuwa chanzo cha msukumo. Mahatma Ghandi aliitumia kama maandiko ya kuhamasisha ukombozi kwa njia ya amani.

Falsafa yake imetaafsiriwa mara nyingi sana—inatafsiri zaidi ya 150 katika lugha kuu za dunia. Leo hii, inachukuliwa kama kitabu cha kiroho cha ulimwengu, si cha wahindu pekee.

Katika toleo lijalo tutaendelea na kitabu kingine.

**Je unafurahishwa na jarida letu?**

**Tuambie kupitia Whatsapp**

**+255 766 974 865**

# KITABU NILICHOSOMA

## KOVU LA MOYO

**Msomaji: Joynice Joseph**
**MWANDISHI wa kitabu ni Mariam Mbano.**

Kovu la moyo ni kitabu ambacho nimekua nikivutiwa kukisoma Mara mbilimbili,na wala sihishiwi hamu kukisoma tena na tena kwa jinsi kilivyo na madini ya kutosha ndani yake. Kovu La Moyo kinamulika uhalisia wa maisha tunayoishi kila siku katika uhusiano wa kimapenzi, binafsi nimejifunza mambo mengi sana, tena kimenifanya niweze kuyakabili na kuyamiliki maisha yangu.
Mwandishi ameelezea namna bora ya kuboresha mawasiliano kwa wapendanao, pia kujijua wewe binafsi na uhusiano ulionao

1.Uhusiano unajengwa na pande mbili, yaani upande wa mwanamke na upande wa mwanaume, kila upande unapaswa kushiriki katika kuujenga uhusiano, ili mahusiano yaweze kua imara,na yenye upendo wa dhati. (Uhusiano ambao unaelemea upande mmoja, huwa hauchukui round kuvunjika hata kufikia kikomo. Mara tu yule ambaye alikua anajenga akichoka basi uhusiano unaishia hapo)

2.Ni muhimu kujadiliana kwa kina, once mnapoingia katika mahusiano, kuhusu ndoto na malengo yenu, ili kuangalia namna bora ya kuyatimiza, bila kuathiri lengo la mmoja wenu.
Mfano kwenye simulizi ya George na Getrude katika kitabu, kila mmoja alikua ana malengo tofauti na mwenzake, Getrude ana biashara ya nguo Dsm huku mpenzi wake anawaza kuwekeza Mbeya awe mkulima mkubwa. Kutofautiana kwa malengo kunaweza kuua kabisa mahusiano, kama George alivyoachana na Getrude.

3.Kujua lugha za mapenzi ambazo mwenza wako anazungumza. Ili uweze kuboresha na kuimarisha uhusiano wenu, Jua mwenza wako nini anapenda kufanyiwa na kipi hapendi, ili kutoziua hisia za mapenzi kati yenu,



Mwandishi ameelezea kitabu Cha THE 5 LOVE LANGUAGE By Gary Chapman, kinaonyesha lugha za mapenzi zipo 5; kama vile kupeana zawadi, kusaidiana kazi nk,

4. Kuzimudu/kuzikabili hisia, kutolipa visasi au kutofanya visa, vurugu, vibwanga na mikasa kwa ex wako, kisa tu umeachwa/au mmeachana. Mfano vile Getrude alivyomuandama bae mpya wa ex wake(Beatrice) hata akafikia hatua ya kumtumia majambazi ili wamzuru.
Na siajabu ndomana George alimwacha kwakua alikua hawezi kujizuia/kukabiliana na hisia zake.

7. Mambo ya kufanya pale penzi lenu linapofika tamati, Tengeneza mfumo mpya wa maisha, achana kabisa kutaka kujua habari za ex wako hazitakusaidia chochote zaidi ya kukuumiza, focus kwenye maisha yako, timiza malengo yako, usikae kizembe fanya shughuli za kukuingizia kipato, lia maliza, vaa pendeza kua smart endelea kujipenda kuwa mtu mwenye furaha,hii itavutia hata watu sahihi kukupenda tena.
Tofauti ukijichukia na kujiacha rafu ukawa mtu wa kulialia tu, hata watu hawawez kukupenda tena mana hujatambua thamani yako. Kovu la moyo kimeeleza jinsi ya kutambua thamani yako.

8. Jipe muda wa kupumzika, Jitulize, usikurupuke, umetoka kuachwa, kuacha, au kuachana leo kesho ushaanza mahusiano mapya, Big noo, kitabu kinaeleza namna ya kujipa muda, pumzika, tumia huo muda kutafakari mahusiano yako yalopita. Basi yale madhaifu yako yafanyie kazi, ni vyema kupumzika atleast 3 up to 6 month ndipo uanze mahusiano mapya, hata akili nayo itakua imerelax,l akin usipojipa muda basi unakua mtu ambaye unamahusiano yasiyodumu, mana haujipi muda wa tathmini.

9. Usirudiane na mtu kwasababu unampenda, mapenzi pekee hayafanyi uhusiano kua Bora, kitabu kinaelezea mambo ya kuzingatia pale unapotaka kurudiana na *ex* wako, na mambo ya kuzingatia kabla hujafanya uamuzi huo, pamoja na mbinu za kurudiana na mpenzi mliyeachana .
Mfano simulizi ya Florida na Sweetbert jinsi walivyorudiana.

R.M

# HABARI PICHA




ANNA MBISE muasisi wa Anna Mbise Mobile Library katika picha ya pamoja na mmoja wa waalimu wa Janice.



Kulia ni Mwenyekiti wa CHAFAMA akikabidhi barua ya utambulisho kwa Mkurugenzi wa Mtalimbo Books Bw. Peter Goima katika ofisi za Mtalimbo, Manzese, D'salaam



ESTER Karin Mngodo (kushoto) akiwa katika hafla ya uzinduzi wa kitabu cha SALAMA BINTI RUBEYA iliyofanyika huko Zanzibar Mwezi Agosti



**TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.**
**Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.**
**Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com**

## PIGA KURA TANZANIA

Uchaguzi Tanzania, Oktoba metufikia
Kila alotia nia, wananchi kafikia
Yote ni kujenga njia, ili kura kumpatia
Piga kura Tanzania, amani dumisha pia.

Haki yako itumie, fika kituo cha kura
Wala usipuuzie, si kula bali ni kura
Umtakaye mpigie, siri ni boksi la kura
Piga kura Tanzania. Amani dumisha pia.

Kampeni sikiliza, na kwa akili chagua
Usibaki kwenye kiza, masikioyo fungua
Hakuna wa kukataza, umtakaye chagua
Piga kura Tanzania, amani dumisha pia.

Vyama vimejitokeza, nafasi kugombania
Watu wamejitokeza, kura kuzipambania
Wengine lao gereza, haki kuipigania
Piga kura Tanzania, amani dumisha pia.

Twaimba demokrasia, nchi yetu Tanzania
Daima twajivunia, amani yetu asilia
Ni haki kutia nia, kwa kila Mtanzania
Piga kura Tanzania, amani dumisha pia

Shime shime kwenu nyote, kutimiza yako haki
Tusipakane matope, wala huyu kudhihaki
Kiti ni chetu sote, asinyimwe mtu haki
Piga kura Tanzania, amani dumisha pia

Si mbali haapo Oktoba, itafute yako kadi
Mana isije koloba, ikakuacha badibadi
Nenda we usiwe zoba, usimwogope wako dadi
Piga kura Tanzania, amaani dumisha pia.

**Shujaa Maneno**
**Bagaamoyo**
**Pwani**

## PAKACHA

Pakacha liso matundu utalipata wapi ndugu yangu?

Pakacha lako na langu
Yote ni mapakacha tangu
Ukisema bovu langu
Lako ni sawa langu
Pakacha kamwe si chungu
Useme watia maji na changu
Pakacha liso matundu utalipata wapi we ndugu?

Tafuta pote upitapo
Mwisho utasema po
Pakacha ulitendapo
Litasitiri makopo
Usizunguke uchokapo
Pakachalo ni lilo hapo
Pakacha liso matundu utalipata wapi we ndugu?

Kama lipo bila tundu
Hilo si pakacha ni chungu
Ukiliona ndugu yangu
Usiache kunipa utungu
Ili nione kwa macho yangu
Mwisho nicheze ritungu
Paakacha liso matundu utalipata wapi we ndugu?

Thubutu!

**Shujaa Maneno**
**Bagamoyo**
**Pwani**

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**


new text
KAMANDA AMATA
OPERESHENI KASHMIR
OPERESHENI KASHMIR
Sasa Kinapatikana kwa Tsh
15,000/=
JIKAMATIE
NAKALA YAKO
DAR ES SALAAM
Duka la Kona ya Riwaya
Kinondoni Morocco
Simu:
0655428085
Zammira


KAMANDA AMATA
MSALITI
"Kamwe hatoki upande wa adui yako"
MSALITI
15,000/=
Kona ya Riwaya
BOOKSHOP
Fika dukani kwetu au wasiliana nasi Kwa Simu
0655 428 085
Mliopo mikoani tunakutumieni.


KINAPATIKANA
ARUSHA
Kinapatikana Kwa Ally Said Shaban, nje tu ya KIMAHAMA Bookshop
Simu: 0757690302 na 0656744390
KAMANDA AMATA
MSALITI
15,000/=
tu
Jipatie Nakala Yako Sasa!


new text
KAMANDA AMATA
OPERESHENI KASHMIR
OPERESHENI KASHMIR
Sasa Kinapatikana kwa Tsh
15,000/=
JIKAMATIE
NAKALA YAKO
ARUSHA
Nje ya Duka KIMAHAMA
Simu
+255 757 690 302
ALLY SAID

# KUTOKA MAKTABA:MAISHA NI MAPAMBANO—12

**Hiki ni kitabu kilichoandikwa miaka mingi sana nyuma. Kiliandikwa ili kiweze kusomwa na watu mbalimbali na kuwekwa kwenye maktaba za vijijini. Tunakitoa kutoka kwenye maktaba yetu ili kukupa uhondo, Ngurumo ya Mwandishi ni kisima cha fasihi chenye hazina iliyotukuka.**

Hataki kusikia upuuzi ule tena! Shughuli za Mpepo zilizidi kupanuka hasa zile zilizomhusu yeye binfsi na familia yake. Kutokana na kupanuka kwa shughuli zake ilimbidi kupunguza baadhi ya kazi za kijiji hasa kusimamia shamba la kijiji kwa vile shamba lake pia lilihitaji huduma kamili ili liweze kutoa mazao mengi na bora.

Muda mwingi aliutumia shambani yeye na mama Tabu pamoja na vijana wengine aliokuwa anaishi nao. Maarifa aliyokuwa akiyapata wakati wa kusimamia shamba la ushirika yalimsaidia sana katika kutunza shamba lake. Mama tabu na vijana walishughulikia sana bustani ya mboga na matunda. Ilikuwa lazima kufanya hivyo kwa sababu mazao ya bustani yalikuwa ya matumizi ya kila siku au ya muda mfupi tofauti na mazao mengine kama vile mahindi, maharage au mhogo: mazao ambayo yangepelekwa kwenye chama cha ushirika cha kijiji kwa mauzo ya baadae. Haikuwa hivi kwa mazao ya bustani. Haya yalihitaji kununuliwa au kuliwa haraka kabla hayajaharibika. Kwa vile yalikuwa yanastawi kwa wingi, hasa nyanya na mchicha, ilibidi kuyauza kwenye soko la kijiji. Hivyo Mpepo ilimlazimu kujenga kibanda chake pale sokoni kwa shughuli hiyo.

Nyumbani kwake alikuwa na miradi mingine ya ufugaji. Alifuga ng'ombe wa maziwa, mbuzi kidogo na kuku. Mifugo hii yote ilihitaji matunzo thabiti. Mpepo na familia yake, badala ya kutafuta kazi ya kufanya, sasa walikuwa wanatafuta muda wa kumudu kazi zao wenyewe. Kila mara Mpepo ilimlazimu kufika kwa wataalamu wa mifugo, wataalamu wa kilimo na wakati huohuo kushiriki kikamilifu katika kamati ya shule ambayo aliipendelea na kutoa michango yake mingi. Hata hivyo hakuacha kutoa michango na kushiriki kwenye kamati ya kijiji au serikali ya kijiji kwa ujumla.

Kuonesha mwamko wake wa siasa , alikuwa anawakatalia walanguzi kuwauzia mazao yake; badala yake alikiuzia kijiji isipokuwa matunda ya bustani. Maziwa vilevile aliyauza kwenye mkahawa wa kijiji na mengine kugawa shuleni kwa bei nafuu ambayo aliita ni ya kurudisha gharama za uzalishaji na wala isiyo na faida . Kutokana na maziwa aliweza kuwalipia watoto wake wote karo na gharama za sare ambazo zilikuwa zikishonwa pale shuleni kama mradi wa shule.

Ingawa Mpepo muda wake ni mchache bado anaendelea kujiwia muda wa burudani. Maelezo yake kuhusu michezo bado yanadhihirisha ushabiki wake kama ilivyodokezwa hapo awali.

"Mbali na kazi nyingi bado ninahitaji mazoezi ya mwili. Zoezi nilipendalo ni lile la 'kuruka kichura! Mimi huchutama na kuruka hapa na pale. Kila siku ambayo huwa nipo mzima lazima nitafute muda wa jioni nirukeruke kwa muda usiopungua nusu saa hadi moyo unapokwenda mbio. kisha hujinyoosha na kujihisi vyema kabisa.

***Itaendelea...***

**Jambo jipya kutoka JAMVI LA SIMULIZI litakujia siku chache zijazo. Stay tuned**

# ELIMU JAMII

## SAFARI YA MALEZI - 04

### 3.0 NIDHAMU KATIKA MALEZI

Nidhamu si adhabu. Ndio kwanza jambo la kuelewa. Si jambo la kumkomoa mtoto kwa kosa alilofanya, bali ni njia ya kumwelekeza apate kutambua thamani ya maamuzi yake. Watu wengi hudhani kuwa ukimpenda mtoto huwezi kumwadhibu, lakini mimi nimejifunza kwamba unaweza kabisa kumpa adhabu mtoto kwa upendo, na hiyo ndiyo adhabu halisi inayolea.

Upendo wa kweli hauachii kila kitu kiruhusiwe, bali huonyesha mpaka na mwongozo. Mtoto anayepokea kila anachotaka, anayesifiwa tu hata katika makosa, anakua bila msingi wa maadili. Lakini mtoto anayeelekezwa, anayekosolewa kwa hekima, na anayepokea maonyo katika mazingira ya upendo, hujifunza kuchambua kati ya jema na baya. Anaelewa kuwa kuna sababu nyuma ya kila onyo, na sababu hiyo ni upendo.

Wazazi wengi wanapokuwa wakali, huamini wanadhibiti. Lakini kuna tofauti kati ya ukali na uthabiti. Ukali hujenga hofu, uthabiti hujenga heshima. Uthabiti wa mzazi au mlezi unapaswa kuja kwa utulivu, si kwa kelele. Kwa mfano, mzazi anaposema kwa utulivu, "***Sitakuruhusu kwenda kwa sababu najua kuna madhara,***" kuliko kupiga kelele na kusema, ***"Hutoki nje kabisa!"*** tofauti ya sauti hizo mbili ni tofauti ya roho mbili: roho ya hofu na roho ya upendo.

**Na. KELVIN JOHN KYARA**

**0753767930**

Nidhamu pia ni fursa ya kukua pamoja. Wakati mwingine, mtoto anapokosea, ni nafasi ya mlezi kujifunza namna bora ya kuelekeza, si sababu ya kumhukumu mtoto milele. Pale tunapoadhibu watoto bila maelezo, tunajenga ukuta. Lakini pale tunapowapa nafasi ya kuelewa kosa, na tunapoweka adhabu yenye maana, tunawajenga kuwa watu wenye msimamo wa ndani.
Nimeona kuwa mtoto anaweza kulia leo, kwa adhabu aliyopata, lakini kesho akakumbuka na kusema, "*Niliambiwa kweli.*" Huo ndio ushindi wa nidhamu ya upendo, haimwumizi mtoto, bali inamfanya kuwa bora. Tofauti na hofu ya kimamlaka, nidhamu ya upendo humfundisha mtoto kuwajibika hata pale mlezi hayupo. Inamfundisha kufikiri, kuchagua, na kubeba matokeo.

Kwa hiyo, katika malezi, upendo na nidhamu havipingani. Badala yake, vinaishi pamoja kama jua na mwanga wake. Huwezi kusema unampenda mtoto na ukamuacha ajiendee hovyo. Na huwezi kumwadhibu kweli bila kumpenda kwanza. Nidhamu ni zawadi ya upendo. Na upendo wa kweli hujua namna ya kutoa zawadi hiyo kwa wakati unaofaa, kwa sauti ya upole, na kwa lengo la kujenga, si kubomoa.

### 3.1 Malezi na adhabu

Katika familia nyingi za Kitanzania, adhabu imekuwa njia kuu ya kurekebisha makosa ya mtoto. Lakini mara nyingi, namna adhabu inavyotolewa huacha madhara makubwa kwa mtoto kuliko faida. Kwa bahati mbaya, adhabu hiyo hutolewa bila kuzingatia haki, huruma, wala uhalisia wa kosa.

Wazazi wengi hasa mama hujenga hofu ndani ya mtoto kwa kutumia jina la baba kama fimbo ya nidhamu. Mara kwa mara mtoto anapokosea, mama humwambia: "*Ngoja baba yako aje, nitamwambia kila kitu,*" hata kama kosa lenyewe ni dogo au lilitokana na kutoelewa. Hili humpa mtoto picha ya baba kama mtu wa kuogopwa, si wa kupendwa. Baba hawi tena sehemu ya faraja, bali anakuwa ni kivuli kizito kinacholeta hofu nyumbani, mtu mkatili.

Na hali huwa mbaya zaidi pale baba anapokuja, na bila kuuliza, bila kuchunguza ukweli, huamua kumpiga au kumwadhibu mtoto kwa hasira kali. Hii ni hatari, kwa sababu mtoto hupoteza imani kwa wazazi wake wote wawili, mama kwa kumtupa kwa hofu, na baba kwa kutokumsikiliza.

Katika baadhi ya familia, adhabu huchukua sura za unyama na mateso. Kwa mfano, mtoto anapochukua shilingi mia mbili (200) iliyokuwa mezani, mzazi anamchukulia kama mwizi mkubwa. Badala ya kumuuliza kwa upole na kumfundisha, mzazi huyo huchukua pasi ya umeme na kumwekea kwenye mkono au mgongo wa mtoto. Wengine hutumia waya wa pasi, vijiti vya mnazi *(chelewa),* au hata mkaa wa moto. Hii si adhabu ya kulea bali ni mateso ambayo huyavunjavunja maisha ya mtoto kwa ndani.

Mtoto anayeadhibiwa kikatili hakui na tabia njema, bali hujenga chuki, woga, na hasira ya ndani. Haoni tena kosa lake, bali anabeba maumivu aliyopitia. Na mara nyingine, anakuwa na kiu ya kulipiza baadaye, au anajifunza kutumia ukatili kwa wengine.

Mzazi wa huruma hutofautisha kati ya adhabu na ukatili. Anaelewa kwamba mtoto hufanya makosa kwa sababu bado anajifunza. Badala ya kutumia fimbo au mateso, mzazi anaweza kutumia mazungumzo, mfano wa maisha, au hata kutenga muda wa mtoto kufikiria makosa yake. *Kulea si kupiga*, *Kulea ni kufundisha*. Na adhabu ya kweli ni ile inayomsaidia mtoto kuelewa kosa lake na kuwa mtu bora zaidi, si ile inayomuumiza hadi kupoteza imani na upendo.

**3.2 Aina bora za adhabu zenye kulea na kusaidia mtoto kukua**

**3.2.1 Adhabu ya mazungumzo (kumuita na kumweleza)**
Badala ya kupiga au kufoka, mzazi humuita mtoto na kuzungumza naye kwa utulivu. Anamweleza kosa lake, kwa nini halifai, na athari zake kwa wengine. Mtoto anajifunza kuwajibika na kuelewa maadili bila woga.

**3.2.2 Kumvua raha fulani kwa muda**
Kama mtoto amekosa nidhamu, mzazi anaweza kumnyima runinga, michezo, au kutumia kitu anachokipendelea zaidi kwa muda fulani. Hii inamfundisha kuwa kila jambo jema lina masharti, na uhuru huja na nidhamu.

**3.2.3 Kuandika au kuomba msamaha (Reflection Punishment)**
Mtoto anaweza kupewa kazi ya kuandika: "*Nitaepuka kusema uongo*," mara 10 au zaidi. Au anaambiwa amwombe radhi aliyemkosea kwa njia ya heshima. Hii hufundisha toba na kuwajali wengine.

**3.2.4 Kuweka mkataba wa tabia (Behaviour Contract)**
Kwa watoto wakubwa, mzazi na mtoto wanaweza kuandikiana makubaliano kuhusu tabia nzuri, malengo, na adhabu zitakazotolewa kama mkataba huo utakiukwa. Inawajenga watoto kuwa na nidhamu ya ndani.

**Mwisho,** malezi bora ni yale yanayojengwa kwa upendo, ambapo nidhamu huongoza mtoto kutenda yaliyo mema. Na adhabu inapotolewa kwa hekima na haki, humfundisha mtoto vyema, bila ya kumvunja moyo na kumjengea chuki. *"mlee mtoto katika njia impasayo naye hataiiacha hata atakapokuwa mzee"*

## SANKARA WA II CHAZINDULIWA




### Kutoka Mkuki na Nyota Publisher

Shukrani nyingi sana kwa wote mliohudhuria uzinduzi wa Sankara wa II cha @lubacha_the_author! Tukio lilikuwa la kipekee na la kusisimua.

Tulipata kusikiliza kipande kifupi cha sauti kilichotupa hamasa ya kutaka kujua zaidi — simulizi ya mhusika mkuu aliyejiita Sankara wa II kwa ujasiri wa kufichua maovu yaliyokuwa yakifanyika.

Ni heshima kubwa kuwa na Balozi Liundi na tunamshukuru sana kwa kuzindua kitabu hiki. Tunawashukuru wote mliojumuika nasi katika uzinduzi huu.

**Kitabu hiki kinapatikana TPH BOOKSHOP Dar es salaam 18,000/= tu**

# HADITHI

## HAPPY NEW YEAR '09'—Twahir Yusuph

*Ilipoishia…*

**Aliipata, akaganda hapo akiipa ambacho hisia zake ilikitaka kutoka kwa mpenzi wake huyo wanayependana. Sekunde chache mbele, ile midomo yao iliyonasana na kupasiana ndimi zao zilizogalagazana kinywani, iliacha. Aibu ndogo zikajipamba kwenye nyuso zao zilizochafuka kwa Ice cream, midomo yao ikitakata na kumeremeta, huku kila mmoja akitabasamu. Hawakukumbatiana saa hii. Walikuwa wakitazamana.**

---

*Endelea...*

"Kesho asubuhi kuna mahali nitaenda, nikitoka nitakufuata mpenzi." Labi akawa wa kwanza kuyafungua tena maongezi.

"Wapi Honey." kwa sauti ya kudeka aliuliza Vivi.

"Mahali tu, kwenye mizunguko yangu ya kawaida kipenzi. Sitakawia."

"Sawa, mi nitakusubiri."

"Okay, kwaheri, nikutakie usiku mwema."

*"You too honey,* nakupenda sana." Vivi aliongea akianza nyanyua hatua na kulifuata geti ambalo walisimama mbele yake.

*"Love you Trillions sweetheart."* alirejesha jawabu Labi, na kumfanya Vivi ageuke na kutabasamu. Hakuondoka Labi, hadi alipomshuhudia Vivi wake akizama getini ndani nyumba hiyo iliyo mbele yake, ndipo aliponyanyua nyayo zake na kutoweka, usafiri wake aliuacha mbali kidogo, ili tu atumie muda wa kufanya matembezi ya kimahaba na Laaziz wake, kopa lilijaa hadi liliviria, sio utani.

*****

Baada ya mikutano miwili aliyoifanya na IGP wake pamoja na mkuu wa majeshi nchini, Inspekta Kasese alikuwa nyumbani kwake saa hii. Pembezoni mwa kitanda chake. Aliketi juu ya kiti huku mbele kukiwa na meza ndogo, fikra zake zikonesha kuwa mbali na mwili wake ulio chumbani akiwa mwenyewe tu. Alizidi kuyatafakari maelezo ya wote wawili kwa kina, lakini kitu alichokidadisi zaidi ni jina la Labi Kimati. Kwanza ni kikao cha kibiashara cha marafiki hao watatu kilichofanyika nyumbani kwake, halafu usiku huohuo mtu mmoja baina yao apoteze maisha. Pili ni kuhusu siku ya msiba, ambayo Labi ilisadikika angeongozana na rafiki yake wa pili marehemu, lakini ghafla akahudhuria peke yake msibani, kisa rafiki yake Imraan alimwambia yeye atachelewa, tena kwa njia ya kutumiana ujumbe, kwanini hakumpigia simu sasa?

Kichwa kilimuuma Inspekta. Aliegesha mgongo wake kitini akikaa kiudadisi zaidi, "hapana, kabla sijafikiria kupindukia, nahitaji kufanya mahojiano na huyu rafiki mmoja aliyebaki hai, napaswa kufanya hivyo siku ya kesho, isipite." alijisemea kwa sauti Inspekta. Kiza kikajitoa angani, jua likachanua kuonesha sasa ni zamu ya utawala wake. Ilikuwa asubuhi, siku ambayo Labi Kimati alimuahidi ayuni wake Vivi kuwa kuna mahali ataenda, lakini hakumtajia jina la sehemu husika. Ndiyo siku hiyohiyo pia, Inspekta Kasese alipanga kufanya mahojiano na Labi Kimati, tena hakutaka ivuke bila kutimia, tayari alishaanza kumtilia mashaka. Siku hiyo inspekta Kasese aliwahi sana kazini, ili kuendelea na uchunguzi wake kabla hajampata Labi na kufanya naye mkutano alioupanga.

**********

Saa mbili asubuhi, ndani ya ofisi yake kituo cha polisi. Akiwa anaendelea na shunguli zake simu yake ilivuma kwa sauti na kumshtua, aliinyanyua mezani alipoiweka na kuitwika viganjani, alikuwa amepokea ujumbe Inspekta Kasese. Aliifungua. *"Nimekutumia picha na maelezo WhatsApp"* ilikuwa ni ujumbe kutoka kwa Domy, kijana wake wa siri. Hakufanya ajizi, moja kwa moja alizama mtandaoni kwenda kutazama alichotumiwa, ni vilevile kama alivyoambiwa. Ilikuwa picha moja inayowaonesha watu watano, Jax, Imraan, Labi pamoja na wengine wawili wenye mionekano ya kuwazidi umri vijana hao watatu. Kwa maelezo ya Domy, yalieleza watu wawili walioongezeka pichani hapo, mmoja ni Daktari na mwingine ni Hakimu. Kilichompa mshawasha zaidi Inspekta Kasese, aliposoma kuwa baina yao wamebaki wawili tu kwenye picha hiyo, Labi pamoja na daktari, huku watatu wakiwa tayari ni marehemu. Tena kifo cha Hakimu kilitokea miaka miwili iliyopita kwa sababu ya maradhi aliyougua muda mfupi tu, na kupelekea kumpora uhai wake. Kingine kilichomsisimua zaidi ni tamati ya maelezo hayo yakisema, Labi Kimati


ameelekea kwa daktari huyo asubuhi hiyo. Yaani muda huohuo ambao Azizi Kasese anasoma jumbe hiyo. *"Ameenda kufanya nini?"* Alijiuliza nafsini Inspekta. *"Watu watano kwenye picha moja, watatu wafe! Hawa waliobaki saa hizi wanaenda kukutana!"* aliendelea kufikiri huku akijiuliza kwa mishangao na udadisi. *"Hapana, nahitaji kuwafuatilia hawa wawili."* Tamati aliona sio rahisi, lazima kutakuwa na chochote baina ya hawa waliobaki, anapaswa kuwapeleleza. Kama wote wawili hawatakuwa wanahusika, basi huenda mhalifu yupo katikati yao, au wao watakuwa wanafahamu chochote kuhusu mauaji ya Jax na Imraan. Aliwaza hivyo, japo binadamu aliyemtilia mashaka zaidi ni Labi Kimati.

Alimwita kijana wake anayemwamini, ni James Kiko, walitoka na kwenda kuanza kazi ya kumfuatilia Labi kimati, pamoja na Daktari aliyeenda kuonana naye. Jumbe alizotumiwa WhatsApp zilimfikia na kila kitu, ziliekeza ni wapi daktari huyo anaishi na hadi namba ya nyumba yake, Domy hakuwa mtu wa masihara hata punje. Alijua anachokifanya. Inspekta Kasese pamoja na afande wake James Kiko walishashika njia tayari, gari ikiwa kasi barabarani, ilizidi kuutawanya upepo kumfuata Labi Kimati, nia ilikuwa kwenda kuyachunguza makutano yake na huyo daktari, picha pamoja na vielelezo vingi alivyopata kuhusu Labi vilimtia wasiwasi inspekta huyo wa polisi. Takribani lisaa limoja mbele, gari yao ikawa imewasili eneo waliloelekezwa na ujumbe ule wa Domy, ni Joha.

Pande wanazoishi mafahari ndani ya nchi ya TAKASENI, mitaa ilikuwa imepangika kwa kuvutia mno, ghasia zikiwa ndiyo kitu kisichojulikana kabisa kwenye kitongoji hicho. Inspekta pamoja na askari wake James Kiko waliteremka garini mwao, taratibu wakaanza kuifuata sehemu husika, ni hatua ishirini hadi kulifikia jengo analoishi Daktari. Waliamua kuiacha gari mbali kusudi. Mbele ya geti la jengo hilo kubwa na kisasa, walifika na kusimama. Inspekta Kasese akagusa kitufe cha kutoa taarifa kuwa kuna ugeni kizuizini huku, mje mtufungulie. Akabinya tena kitufe cha kengele, lakini kimya kikatawala, hawakujibiwa. Hakuchoka, akagonga geti dogo kwa kishindo, ila ajabu lilionesha ishara ya kuwa wazi. Kwanini? Nani kafungua? Na mbona hawajibiwi sasa getini hapo licha ya juhudi zote za kistaarabu wanazofanya!

Hakugonga tena, taratibu alilisukuma geti hilo ili kuhakiki, ndiyo lilikuwa wazi. Walitazamana machoni wakipeana ishara za kipolisi, kila mmoja akaichomoa bastola yake alipoihifadhi, tahadhari zikawajaa, tayari hisia mbaya zilishawafunika ndani ya chandarua cha hatari. "Hodiii" safari hii Inspekta Kasese aliita kwa sauti, lakini bado hakuitikiwa, tayari palionekana hakuna amani tena sehemu hiyo. Kwa tahadhari na umakini mkubwa wakaanza kuingia ndani ya jengo hilo, huku wakiitanguliza midomo ya bastola zao mbele. Walifanikiwa, lakini bado hapasikiki sauti ya kuwemo yeyote, ukimya ulikuwa mkubwa hadi unatisha. Ndani ya jengo, walijitawanya na kuanza ukaguzi kwa kulitanda eneo la nje. Dakika mbili mbele walishalimaliza na kukutana tena uso kwa uso maafande hao wawili.

Kila mmoja alimpa ishara mwenziwe kuwa alikopita pako sawa, palibaki ndani. Taratibu wakausogelea mlango mkuu wa nyumba hiyo, nao ulionesha uwazi kuwa uliegeshwa tu haukufungwa. Hiyo ikazidi kuwapa taarifa nyingi za wasiwasi. Wakawa wanazinyanyua hatua zao kwa tahadhari ya *kiwango cha Corona*, kwani tayari palishaakisi picha mbaya isiyo na amani ndani ya jengo hilo. Wakafanikiwa kuingia, lakini ghafla mboni zao zikashtuliwa kwa kuiona mitapakao ya Damu kiwambazani, tena ikiwa imejichora kwa alama ya viganja vya mikono. Hiyo ikawawasilishia taarifa nyingine isiyo nzuri kwenye vichwa vyao, wakaongeza kujihami. Hatua zao zikaujaza umakini, mboni zao zilipepesa kwa uangalifu mno, huku viganja vyao vikizishikilia vizuri bastola zao.




**Je nini kitaendelea?**

**Tukutane toleo lijalo.**

# RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (04)- Na: Eva Mrema

***ilipoishia***

**Tulipika na kula pamoja, baada ya hapo kila mtu aliaga kwenda kulala. Sijui kuhusu mdogo 'angu, binafsi usiku uligeuka mrefu kuliko barabara iendayo nisipopajua. Kila nilipojaribu kutuliza ubongo Sunche anatawala fikra zangu. Ni wiki mbili za moto sana tangu nilipokutana naye. Yaani ni kama naishi maisha mapya na kuyapuuza ya zamani. Aisee! Nilipatikana nyie! Acha machozi yanibubujike tu.**

---

*Endelea…*

Nilifanya juhudi kwenye kazi na kutumia muda kidogo na Sunche ambaye ailiishi na mimi kwenye kivuli cha urafiki. Mbali na muziki hakuna kitu nilipenda kama kula vizuri. Niliyajua machimbo yote ya misosi jijini. Nilimtembeza bwana Mzungu hadi jiji lilitambua uwepo wetu. Nilizifunga mkanda sana hisia zangu, nilijitahidi mitoko yetu ihusishe maeneo yenye watu. Mara chache nilialika marafiki zangu wa kike tujumuike. Kila aliyetutazama kwa mbali ama kwa karibu alijipa majibu mawili, sisi ni wapenzi au wanandoa. Mawasiliano yetu yaliimarika kama mmea uliopandwa kwenye njia ya chemichemi. Miezi mitatu ya mangojeo ilikuwa kama miaka thelathini ya kusubiri mume atoke vitani. Ndoto pevu zilinisumbua, kama ningeongea na mtaalamu basi ningeonekana namiliki jini mahaba mwenye nguvu za kutosha. Upweke wenye suluhisho usikie tu kwa majirani.

"Kwanini wewe ni dhaifu namna hii? Unakuwa kama mtoto mdogo? Kwani ukimwambia Sunche ni nini kitatokea, jaribu tu! Utateseka hata lini? Utalilia mapenzi mpaka lini? Kamwambie basi. Akheri akukatae ukate tamaa kuliko hivi" nilizungumza na mtu kwenye kioo changu. Niliongea na taswira yangu. Nilijihurumia na kuumia kwa ajili yangu kwa wakati mmoja. Ni muda ambao nilikuwa kama nilivyozaliwa. Nilitoka kukoga. Nilijikausha maji mwilini, kwa kutumia kanga, Nilivaa nguo yangu ya bahati. Ndio ni nguo ambayo kila mara niivaapo jambo zuri hunitokea. Kuna mtu kataja rangi huko? Nyeupe! Ndio ni gauni langu jeupe, la mpira mzito, huku tunaziitaga kaba shingo. Ni fupi ya wastani wa kutosha kukwambia sina miguu mibaya. Miguu yangu ni mfano wa zile bia za kizamani. Ilikuwa mizuri atii!

Nilitoka na malengo mawili. Lengo namba moja ni kuhudhuria siku kuu ya kuzaliwa ya mpenzi wa rafiki yake Sunche ambayo tulialikwa. Jambo la pili ni kuisikiliza na kuitii ile sauti inayonifokea. Nilipanga kuzianika hisia zangu kwa Sunche. Nilibadili mpango wa kungojeana. Nilimuomba tukutane kwenye tafrija. Nilimtangulia kufika. Nilitafuta kona nzuri nikaketi. Wageni waalikwa, ndugu wachache na marafiki walitimba kwa kupokezana. Burudani ilishika hatamu. Nilikaa kinyonge sana, Sunche hakuwa kafika. Ulifika wakati wa kuimba mubashara. Waliimba walengwa wenye sherehe yao. Waliimbiana kimapenzi kiasi niliburudika moyoni. Nilitamani kuimba. Nilisuuza koo na kukiomba kipaza sauti. Kwakuwa nilivaa viatu virefu, basi kuketi ilikuwa wazo kabambe. Nakuwa huru nikiimba nyimbo za kizungu maana ndizo nasikiliza zaidi. Za Kiswahili napenda za Injili, au za taratibu za mapenzi ambazo zilikuwa chache.

Chaguo langu usiku huu ni wimbo wangu pendwa kabisa ulioimbwa na kundi maarufu duniani, lijulikanalo kama 'West life'…jina la wimbo, *I wanna grow old with you*'. Nilianza taratibu na kupanda kwa kufuata ala za mapigo yake. Niliimba kama fundi kwenye mashine yake. Nilifanya kama Jini Kinyonga kwenye ushairi. Nikapiga kama Mr. Romantic kwenye kuyaghani mapenzi. Niliimba. Na kama bahati ya mtende kuota jangwani, niliyemuimbia akatia timu bila ajizi. Alikuja nilipokuwa na kunikabidhi maua ambayo sina uhakika kama yalikuwa yangu tokea mwanzo au ilikuwa zawadi ya mwenye

**RIWAYA: NGUVU YA KIAPO**

Inapatikana katika kitabu (nakala ngumu) na soft copy (nakala tepe) kwa bei ya kirafiki.

**KITABU** - Tsh 10,000
**Dar es salaam:**

- Duka la Kona ya Riwaya - 0655428085
- Kalamu Tulivu Magomeni - 0718975659
- Posta Mpya kwa Joji - 0713454152
- Temeke kwa Eva Mrema - 0742630141

Soft Copy (Nakala tepe) PDF - Tsh 5,000
'Offer' kupitia Ngurumo ya Mwandishi ni - Tsh 3,000
Lipa kwa **MPESA LIPA NAMBA 36499709 Eva John Mrema**

# RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (04) - Na: Eva Mrema

shughuli yake.
Alinyoosha mkono kuninyanyua na kunitaka tucheze ningali ninaimba. Nilisimama na kuyaketisha maua kwenye kiti nilichokuwa nimekalia. Niliutoa mkono na ushirikiano wangu wote. Tulicheza hali binafsi nikiimba. Muda wote nilimtazama usoni, nilitamani aelewe tu kile naimba, basi natamani kijiri kwetu.
Ubeti wa mwisho niliuimba nikiyapapasa mashavu yake kwa kumaanisha haswaa! Na nilipomaliza kuimba, sikungoja nijishauri… "Sunche, nakupenda" niliitamka sentensi hiyo iliyonifanya nihisi miguu kukanyagana na moyo kukosa utulivu. Ni hivii! Nilitamka bwana. Nilimwambia Sunche nampenda. Baada ya kutamka kila kiumbe hai eneo lile kilinishangaa, lakini Sunche hakufanya hivyo.

Aliondoka kwa haraka bila kusema neno lolote. Alitoweka kabisa eneo lile. Miguu yangu haikuwa na nguvu hata za kumkimbilia. Machozi ambayo sikuwa nimekubaliana nayo yakaanza kuchuruzika mashavuni. Sikuwa na mtu niliyemzoea kati ya wote waliokuwepo. Niliwahi kuonana na rafiki yake mwenye tafrija mara moja tu, hata jinale sikuwa nimelikariri. Nilijikaza na kuyayuka pale mbele jukwaani. Nilipiga hatua za polepole kuelekea msalani. Nilipofika, sikuingia kujisaidia nilibaki nimesimama kwenye kioo nje ya milango mingi ya choo kile. Sikujizuia tena mbele ya kioo kilichonifanya nitazamane na uso wa mwanamke ambaye sikuwahi kumbaini ndani yangu. Nilionekana dhaifu na nisiye na tumaini. Nilitia sana huruma. Nililia mno na mara hii nililia huku najitazama.


Nililia nikizungumza na nafsi yangu dhaifu iliyoniadhibu. Nakwambiaje! Nililia kama kinda la ndege lililotelekezwa na mamaye ugenini. Niliulaumu ulimi kwa kufanya mambo yangu kuwa magumu. "Kwanini nilisema sasa? Kwanini yani! Ningenyamanza ningepungukiwa na nini atii! Nimeharibu na kujidhalilisha mno, nikaage niende nyumbani sasa inatosha" nilijisemesha kimyakimya.
Niliukosha uso wangu kisha nikaukausha kwa leso niliyokuwa nayo papo, nikarejea ukumbini. Watu walikuwa mchakamchaka kuchukua chakula. "Mpendwa naondoka , nashukuru mno kwa mwaliko na binafsi, naomba radhi kama nilisababisha kadhia yoyote, nawatakia heri na fanaka zote" nilitoa zawadi mkobani na kumpatia mrembo yule, kisha nikamwambia, "*happy birthday once again*"
Nilianza kuondoka, rafiki wa Sunche alirudi kutoka kuchukua chakula na kuniona. Alinifuata huku akiniita jina, kwakuwa mziki uliyateka masikio yangu, sikumsikia. Hakukata tamaa, alinifuata hadi nje na kuniomba nirejee japo nikatie suna ya maakuli. Alining'ang'ania mithili ya ruba. Nikang'ang'anika. Nilirudi na kwenda kuketi na *'birthday girl'* rafiki wa Sunche aliniletea vitafunwa na nyama. Nilikula japo moyo ulinijaa mno. Nilipotezea hisia za uchungu kila niliposikia mziki nilioufurahia. Nilijikuta nikitumia muda mwingi sana kwenye kula shauri ya kula huku naimba.

Ghafla muziki ulizimwa. Taa na nuru vilitoweka. Tuliamini umeme umekatika, kila mmoja alistaajabu maana sio kawaida hali hii kutokea kwenye kumbi za hadhi ya kati. Nilikomaa kutafuta simu yangu mkobani bila mafanikio. Ilikuwa sekunde mia na sitini lakini kelele zake kama tumekaa gizani wiki nzima. Taa ziliwashwa, na kila kitu kikarejea katika hali yake ya kawaida. Simu yangu kumbe ilikuwa mezani kando ya sahani ya vitafunwa. Niliishika na kutaka kuangalia jambo. Lakini kabla, sauti ilisikika. *"Tabita I'm sorry! Will you please be my fiance?"* Sauti ilimtangulia mwenye nayo ambaye alifanya mshangao wa ainaye unipate Tabita mie kwa makusudi kabisa.

"Sijawahi panga kucheza na hisia zako. Natamani kila mtu ajue leo nilifanya kiapo. Kiapo changu kilinifunga kuchukua hatua ya kwanza kwa mwanamke hata kama hisia zangu zilikuwa juu sana kwake. Kiapo changu kimeniletea mtu sahihi maishani na mtu huyo ni wewe Tabita. Nakupenda sana. Natamani leo hii kila anayenijua ajue kuwa niko penzini. Nitaridhia unipige hata vibao kwa mikono yako laini. Nitaridhia hata useme ulinitania tu. Mimi Sunche nakupenda sana bibie" sauti ilitamatika na kiwiliwili cha mwenye nayo kikaanza kujitokeza taratibu jukwaani. "Nikiambiwa niandike shairi juu ya uzuri wako, pengine halitapimika kwa mizani mizuri ya kiandishi, lakini nataka kuweka kumbukumbu hii moyoni mwako….
Kwenye sifa kumi za mwanamke niliyemuota, umeongeza mpya ambayo sikuwahi kuiota.

*Itaendelea...*

# Tangazo




Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi
jamvilasimulizi@gmail.com